**SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR**

# HOTUBA YA WAZIRI WA AFYA
# MHESHIMIWA NASSOR AHMED MAZRUI

# KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

***Mei, 2022***

## YALIYOMO


***Mada*** — ***Ukurasa***

Maelezo ya Vifupisho ........................................................................ iii
UTANGULIZI ........................................................................................ 1
UTEKELEZAJI WA KIFEDHA KWA MWAKA 2021/2022 .......................... 2
MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MALENGO KWA MWAKA 2021/2022..... 5
PROGRAMU YA KINGA NA ELIMU YA AFYA (PH0301) .......................... 6
Huduma Shirikishi za UKIMWI, Homa ya Ini, Kifua Kikuu na Ukoma 6
Huduma za Kumaliza Malaria Zanzibar............................................ 8
Huduma Shirikishi za Afya ya Uzazi na Mtoto ................................. 10
Uratibu wa Shughuli za Kinga Udhibiti wa Maradhi ya Miripuko na Ufuatiliaji wa Maradhi ............................................................ 11
Huduma za Maradhi Yasiyoambukiza............................................ 12
Huduma za Maradhi Yasiyopewa Kipaumbele................................. 14
Huduma za Lishe............................................................................ 14
Huduma za Msingi za Matibabu ya Macho..................................... 14
Huduma za Utoaji wa Elimu ya Afya............................................... 15
Huduma za Afya ya Mazingira......................................................... 16
Huduma za Afya Bandarini.............................................................. 17
Huduma za Afya ya Wafanyakazi.................................................... 18
Huduma za Afya ya Msingi ya Akili................................................. 18
PROGRAMU YA TIBA (PH0302)........................................................... 20
Programu Ndogo ya Huduma za Matibabu (SH030201)................... 20
Huduma za Damu Salama............................................................... 21
Huduma za Mabaraza ya Kitaaluma............................................... 22
Huduma ya Upatikanaji, Uhifadhi na Usambazaji wa Dawa na Vifaa vya utibabu.............................................................................. 22
Huduma za Tiba Asili na Tiba Mbadala.......................................... 23
Programu Ndogo Huduma za Uchunguzi (SH030202) ...................... 24
Huduma za Chakula, Dawa na Vipodozi......................................... 24

Huduma za Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ....... 25
PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA (PH0305) 25
Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji (SH030501) ........ 25
Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti (SH030502) ...... 27
Taasisi ya Utafiti wa Afya ........................................................ 29
Programu ndogo ya Uratibu wa Wizara ya Afya
Pemba (SH030503) ................................................................. 29
PROGRAMU YA HOSPITALI YA MNAZI MMOJA (H02) ..................... 30
Programu Ndogo ya Uchunguzi na Matibabu (SH0201) ............ 30
Programu Ndogo ya Uongozi na Utawala (SH0202) ................. 32
UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO .................................... 33
Ujenzi wa Maabara ya Uchunguzi ya Chakula, Dawa na Vipodozi 33
Ujenzi wa Maabara ya Uchunguzi wa Virusi - Binguni .............. 33
Utekelezaji wa Miradi ya IMF ................................................... 34
Mradi wa Kupandisha Hadhi Hospitali ya Mnazi Mmoja ............ 35
Ujenzi wa Hospitali ya Wagonjwa wa Akili ................................ 35
Ujenzi wa Hospitali ya Wete ..................................................... 36
Ujenzi wa Wodi ya Mama na Mtoto Hospitali ya Chake Chake . 36
Ujenzi wa nyumba za Wafanyakazi Hospitali ya Abdalla Mzee 36
MWELEKEO WA BAJETI NA VIPAUMBELE VYA WIZARA KWA MWAKA 2022/2023 ........................................................................... 37
SHUGHULI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA NA WIZARA YA AFYA KWA MWAKA 2022/2023 ..................................................................... 37
PROGRAMU YA KINGA NA ELIMU YA AFYA (PH0101) ...................... 38
PROGRAMU YA TIBA (PH0102) ...................................................... 38
PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA (PH0103) 40
PROGRAMU YA HOSPITALI YA MNAZI MMOJA (H02) .................... 40
SHUKRANI ..................................................................................... 42
HITIMISHO ..................................................................................... 44
MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2022/2023 ............................. 44

## MAELEZO YA VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| AMREF | - | Africa Medical Research Foundation |
| BADEA | - | Arab Bank for Economic Development in Africa |
| CCM | - | Chama cha Mapinduzi |
| CDC | - | Center for Disease Control and Prevention |
| DNA | - | Deoxyribonucleic Acid |
| EAC | - | East African Community |
| ECHO | - | Echocardiography |
| e-IDSR | - | electronic Integrated Disease Survaillance and Response |
| e-LMIS | - | electronic Logistic Management Information System |
| GFATM | - | Global Fund to Fight AIDS, Tuberculosis and Malaria |
| HSSP IV | - | Health Sector Strategic Plan IV |
| JHPIEGO | - | Johns Hopkins Program for International Education in Gynaecology and Obstetrics |
| MRI | - | Magnetic Resonance Imaging |
| MUHAS | - | Muhimbili University of Health and Allied Sciences |
| NIMR | - | National Institute for Medical Research |
| PEPFAR | - | President’s Emergency Plan for AIDS Relief |
| PMI | - | President’s Malaria Initiatives |
| RCH | - | Reproductive and Child Health |

| | | |
|---|---|---|
| TB | - | Tuberculosis |
| TV | - | Television |
| UAE | - | United Arab Emirates |
| UNDP | - | United Nations Development Program |
| UNFPA | - | United Nations Population Fund |
| UNICEF | - | United Nations International Children Emergency Fund |
| USAID | - | United States Agency for International Development |
| VVU | - | Virusi Vya UKIMWI |
| WHO | - | World Health Organization |
| ZBS | - | Zanzibar Bureau of Standards |
| ZFDA | - | Zanzibar Food and Drug Agency |
| CTCs | - | Care and Treatment Clinics |
| ARV | - | Anti-Retroviral Virus |
| BOQ | - | Bill of Quantities |
| IMF | - | International Monitory Fund |
| ZOP | - | Zanzibar Outreach Program |
| UNDP | - | United Nation Development Program |

## UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** kwanza kabisa naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma aliyeumba mbingu na ardhi na vyote viliomo baina yake, kwa kutujaalia uhai, uzima na afya njema; hali iliyopelekea kukutana katika kikao hiki kujadili bajeti ya Wizara ya Afya.

2. **Mheshimiwa Spika**, Aidha, natoa shukrani za pekee kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi **Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi** kwa kuendelea kuliongoza vyema Taifa hili katika hali ya amani na utulivu. Pia, niwapongeze **Mheshimiwa Othman Masoud Othman** Makamo wa Kwanza wa Rais na **Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdullah** Makamo wa Pili wa Rais kwa mashirikiano mazuri wanayompatia katika kuiongoza nchi yetu.

3. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inatambua na kuthamini mchango mkubwa wa Wajumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii inayoongozwa na **Mheshimiwa Mohammed Ahmada**, hivyo nachukua fursa hii kuwashukuru wajumbe wa Kamati hii kwa namna walivyoshirikiana nasi wakati wote walipofanya ziara katika Wizara hii, wameonesha uweledi na ukomavu mkubwa katika kutupatia maelekezo, ushauri na mapendekezo ya kuimarisha utendaji kwa nia ile ile ya kufikia malengo ya Serikali ya Awamu ya nane (8).

4. **Mheshimiwa Spika,** nichukuwe fursa hii kukupongeza wewe binafsi, kwa kuendelea kuliongoza Baraza hili kwa umakini kabisa. Pia nawapongeza Naibu Spika, Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma na Mwenyekiti wa Baraza hili Mheshimiwa Mwanaasha Khamis Juma kwa kukusaidia katika kuendesha mijadala ndani ya Baraza hili, kazi ambayo wameifanya kwa umahiri mkubwa. Aidha, nampongeza Katibu wa Baraza la Wawakilishi, Ndugu Raya Issa Msellem kwa kusimamia na kufanikisha shughuli za Baraza kwa ufanisi.

5. **Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo sasa kwa ruhusa yako naomba nieleze utekelezaji wa Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kama ifuatavyo:-

## UTEKELEZAJI WA KIFEDHA KWA MWAKA 2021/2022

6. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022**,** Wizara ya Afya, (**Fungu H03**) (kabla kutenganishwa na Idara ya Ustawi wa Jamii na Wazee na Idara ya Jinsia na Watoto) ilikadiriwa kutumia shilingi **197,868,500,000** zikijumuisha shilingi **36,577,900,000** kwa ajili ya mishahara; shilingi **51,809,508,000** kwa kazi za uendeshaji wa ofisi; shilingi **4,385,000,000** kwa ruzuku na shilingi **105,096,092,000** kwa kazi za maendeleo. Aidha, hospitali ya Mnazi Mmoja (Fungu H02) ilikadiriwa kutumia shilingi **20,371,200,000;** zikihusisha shilingi **14,808,900,000** kwa ajili ya mishahara na shilingi **5,562,300,000** kwa kazi za uendeshaji wa hospitali.

7. **Mheshimiwa Spika,** baada ya kutenganishwa na Idara ya Ustawi wa Jamii na Wazee na Idara ya Jinsia na Watoto matarajio ya matumizi kwa Wizara ya Afya pekee (Fungu H03) ni jumla ya shilingi **182,863,195,000**. Kati ya hizo shilingi **35,261,260,000** kwa ajili ya mishahara, shilingi **42,020,843,000** kwa ajili ya matumizi ya uendeshaji, shilingi **4,385,000,000** kwa taasisi zinazopewa ruzuku na shilingi **101,196,092,000** kwa kazi za maendeleo.

8. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2022, Wizara ya Afya baada ya kutenganishwa na Idara ya Ustawi wa Jamii na Wazee na Idara ya Jinsia na Watoto (H03) iliingiziwa jumla ya shilingi **75,179,307,174** sawa na asilimia **41.1** ya makadirio kwa mwaka 2021/2022. Kati ya hizo shilingi **27,563,725,625** kwa ajili ya mishahara (asilimia **36.6**), shilingi **13,717,249,380** matumizi ya uendeshaji (asilimia **32.6**) na shilingi **403,146,213** kwa ruzuku (asilimia **33**). Aidha, shilingi **33,495,185,956.39** asilimia **33.1**), ziliingizwa kwa kazi za maendeleo, kati ya hizo shilingi **4,724,064,155.76** kutoka serikalini, shilingi **4,357,638,389.12** ni ruzuku kutoka kwa washirika wa maendeleo na shilingi **24,413,483,411.51** mkopo wa IMF.

9. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa hospitali ya Mnazi Mmoja shilingi **12,398,722,000** zilipatikana na kutumika. Fedha hizo zinajumuisha shilingi **1,650,724,000** kwa matumizi ya kawaida (asilimia 29.7) na shilingi **10,747,998,600** (asilimia 72.6) kwa ajili ya mishahara. Kiambatisho 1 kinatoa ufafanuzi.

10. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Afya (Fungu H03) kabla ya kutenganishwa na Idara ya Ustawi wa Jamii na Wazee na Idara ya Jinsia na Watoto ilikadiriwa kukusanya shilingi **5,038,053,000** na Hospitali ya Mnazi Mmoja ilipangiwa kukusanya shilingi **1,379,800,000**. Makadirio ya makusanyo ya Wizara ya Afya (Fungu H03) baada ya kutenganishwa ni shilingi **4,137,953,000** na kwa hospitali ya Mnazi Mmoja yamebaki kama yalivyokuwa awali.

11. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2022, jumla ya shilingi **32,970,142,624** (zaidi ya asilimia 100) zilikusanywa kutoka katika vyanzo vya Wizara (H03). Ongezeko hili linatokana na makusanyo yaliyotokana na ugonjwa UVIKO 19. Aidha, shilingi **589,437,730.48** sawa na asilimia **42.7** zilikusanywa na Hospitali ya Mnazi Mmoja. Kiambatisho namba 2 kinatoa ufafanuzi.

12. **Mheshimiwa Spika,** fedha zilizotengwa zilipangwa kufanikisha utekelezaji wa vipaumbele vya Wizara kwa mwaka wa fedha wa 2021/2022 ambavyo ni:-
    i. Kuimarisha huduma za afya ya mama na mtoto ili kupunguza vifo vinavyotokana na uzazi;
    ii. Kuimarisha uwezo na utayari wa kupambana na maradhi ya mripuko na majanga ya kiafya;
    iii. Kuongeza nguvu katika usimamizi wa miradi ya maendeleo;
    iv. Kusimamia utekelezaji wa sheria na taratibu zilizowekwa zikiwemo za manunuzi;
    v. Kuendelea na jitihada za kutokomeza ugonjwa wa Malaria Zanzibar;
    vi. Kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa vya utibabu na uchunguzi;

vii. Kuweka mfumo endelevu wa kugharamia huduma za afya;
viii. Kuendelea na hatua za kuanzisha bima ya afya;
ix. Kuimarisha nguvu kazi, kusimamia utendaji pamoja na kuandaa mazingira mazuri ya kazi;
x. Kuimarisha mapambano dhidi ya vitendo vya ukatili kwa wanawake na watoto;
xi. Kuimarisha hifadhi ya jamii kwa wanaoishi katika mazingira magumu;
xii. Kuendeleza mapambano dhidi ya maradhi ya kuambukiza na yasiyoambukiza.

## MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MALENGO KWA MWAKA 2021/ 2022

13. **Mheshimiwa Spika,** yafuatayo ni baadhi ya mafanikio yaliyopatikana na Wizara kwa kipindi cha Julai,2021 hadi Machi, 2022 kama yanavyofafanuliwa katika vifungu vinavyofuata.

i. Kukamilika kwa muongozo wa rufaa kwa wagonjwa katika ngazi zote za utoaji wa huduma;
ii. Kukamilika kwa Mpango Mkakati wa Nne wa Wizara
iii. Kukamilika kwa mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini (Monitoring & Evaluation Framework);
iv. Kukamilika kwa Mpango Mkakati wa Taarifa za Afya;
v. Kuvuka malengo ya dunia ya kufikia shabaha ya 90 tatu katika mapambano ya UKIMWI;
vi. Kukamilika kwa hospitali ya wagonjwa wa Akili Kidongo Chekundu;
vii. Kuipandisha hadhi hospitali ya Micheweni kutoka hospitali ya Kijiji na kuwa hospitali ya Wilaya;
viii. Kukamilika kwa jengo la maabara ya Wakala wa Chakula na Dawa huko Mombasa;

ix. Maendeleo mazuri ya ujenzi wa hospitali 10 za wilaya na hospitali moja ya Mkoa;
x. Hospitali ya Abdalla Mzee imepatiwa mashine mpya ya CT - Scan pamoja na mtaalamu wa mionzi;

14. **Mheshimiwa Spika,** mafanikio haya na mengineyo yanaelezwa kwa kina katika utekelezaji wa shughuli zilizofanyika kupitia huduma zinazotolewa katika kila programu husika kama ifuatavyo: -

## PROGRAMU YA KINGA NA ELIMU YA AFYA (PH0301)

15. **Mheshimiwa Spika,** jukumu la programu hii ni kuhakikisha jamii inapata huduma bora za kinga pamoja na kuongeza uelewa juu ya njia za kujikinga na maradhi ya kuambukiza na yasioambukiza. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, kiasi cha shilingi **34,570,812,000/=** sawa na asilimia 17 ya fedha zote zilitegwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za programu hii. Hadi kufikia Machi 2022 Programu hii iliingiziwa kiasi cha shilingi **10,608,924,973/=** sawa na asilimia 30.7 ya fedha zilizotengwa. Huduma zifuatazo zilitekelezwa kupitia programu hii.

### Huduma Shirikishi za UKIMWI, Homa ya Ini, Kifua Kikuu na Ukoma

16. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara ilitenga jumla ya shilingi **7,221,572,033**, kati ya hizo shilingi **1,000,000,000** ni kutoka Serikalini na shilingi **6,221,572,033** kutoka kwa washirika wa maendeleo. Hadi kufikia Machi 2022, huduma hii imepokea kiasi cha shilingi **2,052,334,569** kutoka kwa washirika wa maendeleo sawa na asilimia 28.

17. **Mheshimiwa Spika,** kuanzia Julai,2021 hadi Machi,2022 watu **252,807** (wanawake **138,625** wanaume **114,182**) walichunguzwa virusi vya UKIMWI. Kati yao watu **1,759** (wanawake **1,180** wanaume **579**) sawa na asilimia 0.6 wamegundulika na maambukizi ya VVU. Aidha, watu **7,721** (wanawake **5,318** wanaume **2,403**) wanaoishi na VVU wameanzishiwa huduma kwenye kliniki 14 (Unguja 10 na Pemba 4) za huduma na tiba (CTCs). Miongoni mwa watu hao; **7,644** (wanawake **5,266** na wanaume **2,378**) sawa na asilimia 99 wanatumia dawa za kupunguza makali ya VVU (ARVs).

18. **Mheshimiwa Spika,** wajawazito **35,007** waliohudhuria kliniki kwa mara ya kwanza walipatiwa huduma ya upimaji wa VVU, ambapo wajawazito **263** sawa na asilimia **0.7** waligunduliwa na maambukizo na wote walipewa dawa za ARVs. Vile vile, watoto **101** waliozaliwa na mama wenye maambukizi ya VVU walichunguzwa kwa kipimo cha DNA-PCR, ambapo watoto wanane (**8**) wameonekana na maambukizi ya VVU na wanaendelea matibabu.

19. **Mheshimiwa Spika,** katika ufuatiliaji wa wagonjwa wa UKIMWI waliopo katika matibabu; jumla ya sampuli za damu **5,472** zimekusanywa na kuangaliwa kiwango cha VVU katika Hospitali za Mnazi Mmoja, Kivunge na Chake Chake. Kati ya sampuli zilizochunguzwa, sampuli **5,113** sawa na asilimia **93.4** zimeonekana kuwa na kiwango cha chini ya kopi **1,000** za virusi na kufikia lengo la kimataifa la asilimia 90 ya kufubaza kiwango cha virusi "Viral Load Supression".

20. **Mheshimiwa Spika,** jumla ya watu **22,686** walichunguzwa virusi ya homa ya Ini B (wanawake **18,964** - wanaume **3,726**) kati yao watu **241** (wanawake **89 -** wanaume **152**) waligundulika kuwa na maambukizi ya homa ya Ini 'B' Unguja na Pemba. Aidha, watu **8,241** (wanawake **2,979 -** wanaume **5,262)** walipimwa virusi vya homa ya ini C ambapo watu **34** sawa na asilimia **0.2** (wanawake **2 -** wanaume **32**) waligundulika na maambukizi.

21. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Kifua Kikuu wagonjwa wapya **1,090** (Unguja **708** na Pemba **382**) waligundulika na Kifua Kikuu na kuanzishiwa matibabu. Vile vile, wagonjwa wa Ukoma **89 (**Unguja **82,** Pemba **7)** wamegundulika na kuanzishiwa matibabu.

**Huduma za Kumaliza Malaria Zanzibar**

22. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara ilitenga jumla ya shilingi **3,564,374,707**, kati ya hizo shilingi **713,545,000** ni kutoka Serikalini na shilingi **2,850,829,707** kutoka kwa washirika wa maendeleo. Hadi kufikia Machi 2022 huduma hii imepokea kiasi cha shilingi **5,847,518,584** kutoka kwa washirika wa maendeleo sawa na asilimia 71, Fedha za ziada zilitolewa na washirika wa Maendeleo katika kukabiliana na UVIKO-19 ni jumla ya shilingi **3,889,861,200**.

23. **Mheshimiwa Spika,** mpango wa kutokomeza Malaria Zanzibar unaendelea kwa utekelezaji wa mikakati mbali mbali ili kufikia azma hiyo. Jumla ya mahudhurio ya watu **636,131** (Unguja **550,752** - Pemba **85,379**); walichunguzwa vimelea vya malaria ukilinganisha na watu

**440,715** waliochunguzwa katika kipindi kama hiki mwaka 2020/2021. Matokeo ya uchunguzi yamebainisha kwamba watu waliogunduliwa na Malaria wamepungua kutoka **6,626 (1.5%)** mwaka 2020/2021 hadi watu **2,780** sawa na asilimia **0.6** mwaka 2021/2022. Katika hatua nyengine, wagonjwa **1,875** sawa na asilimia **89** walifuatiliwa majumbani kwa lengo la kuangalia chanzo cha maambukizo yao. Kiambatisho **namba 3** kinatoa ufafanuzi.

24. **Mheshimiwa Spika,** wilaya inayoongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya kiwango cha malaria ni Magharibi 'B' ikifuatiwa na Wilaya ya Mjini ambapo Wilaya ya Mkoani imeripotiwa kuwa na maambuki ya chini ya malaria. Zoezi la ugawaji wa vyandarua vyenye dawa ya muda mrefu kwa jamii lilifanyika katika Shehia **335** (Unguja **206** na Pemba **129**) ambapo vyandarua **727,872** (Unguja **441,032** - Pemba **286,840**) sawa na asilimia **97** viligawiwa. Aidha, vyandarua **69,753** (Unguja **41,968** - Pemba **27,785**) viligawiwa kwa mama wajawazito na watoto chini ya umri wa mwaka mmoja.

25. **Mheshimiwa Spika,** zoezi la upigaji dawa ya Malaria lilifanyika katika shehia **39** (Unguja **14** na Pemba 25), ambazo zimeonekana kuwa na maambukizi makubwa zaidi. Nyumba **18,697** (Unguja **11,975** na Pemba **6,722**) zilipigwa dawa na kufanikiwa kwa asilimia **97**. Vile vile, Wizara imefanikiwa kuweka viuatilifu vya kuua viluilui vya mbu katika madimbwi (mazalia ya mbu), jumla ya madimbwi makubwa **161** (Unguja **61** na Pemba **100**) yenye kutuwama maji kwa zaidi ya miezi minne yamewekewa viuatilifu. Kiambatisho

**Huduma Shirikishi za Afya ya Uzazi na Mtoto**

**26.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara ilitenga jumla ya shilingi **3,630,199,043,** kati ya hizo shilingi **1,000,000,000** ni kutoka Serikalini na shilingi **2,630,199,043** kutoka kwa washirika wa maendeleo. Hadi kufikia Machi 2022 huduma hii imepokea kiasi cha shilingi **1,500,000,000** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo sawa na asilimia 41 ya fedha zilizotengwa**.**

**27.** **Mheshimiwa Spika,** jumla ya mama **47,195** walihudhuria kliniki ya wajawazito angalau mara moja katika kipindi cha ujauzito ukilinganisha na kina mama **46,050** walioripotiwa mwaka jana katika kipindi kama hiki. Wajawazito wanaojifungulia katika hospitali na vituo vya afya wameongezeka kutoka **33,057** hadi **37,212** (hospital 30,597 na Vituo vya afya 6,615). Hata hivyo, kumekuwa na ongezeko la vifo vitokanavyo na uzazi kutoka **44** na kufikia vifo **50**. Aidha, vifo vya watoto wachanga vimeongezeka kutoka **1,201** na kufikia **1,363** (894 walizaliwa wafu) kwa kipindi cha Julai,2020 hadi Machi,2021. Nachukua fursa hii kuwaomba mama wajawazito kuhudhuria kliniki mara tu wanapohisi dalili za ujauzito sambamba na kujifungulia katika vituo vya afya. Kufanya hivyo kutasaidia sana katika kugundua vihatarishi mapema na pia kupunguza magonjwa na vifo vinavyotokana na uzazi pamoja na vifo vya watoto wachanga. Kiambatisho **namba 4** kinatoa ufafanuzi.

**28.** **Mheshimiwa Spika,** watumiaji wa njia za kisasa za uzazi wa mpango wamepungua kutoka kina mama **63,261** kwa kipindi cha Julai,2020 hadi Machi, 2021 na kufikia **61,379** kwa kipindi kama hiki mwaka 2021/2022. Natumia fursa

hii kuwaomba wajumbe kuhamasisha jamii kupitia vikao mbali mbali katika majimbo ili tufikie lengo la dunia la kuwafikia watu wote wanaopaswa kutumia uzazi wa mpangilio ifikapo mwaka 2030.

29. **Mheshimiwa Spika,** katika kukabiliana na magonjwa yanayozuilika kwa chanjo, Wizara imetoa chanjo kwa watoto chini yaumri wa mwaka mmoja. Jumla ya watoto **41,386** sawa na asilimia **85** walipatiwa chanjo ya Penta 3. Kwa upande wa chanjo ya saratani ya mlango ya kizazi kwa wasichana wenye umri wa miaka **14,** wasichana **5,501** walipatiwa huduma hiyo kwa dozi ya kwanza na **4,298** walipata dozi ya pili.

30. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyengine, watu **174,945** (asilimia 28.1) kati ya watu **622,000** waliotarajiwa kuchanjwa hadi kufikia juni 2022 walipatiwa chanjo tofauti za UVIKO -19, watu **368,592** wamepatiwa chanjo ya kipindupindu awamu ya kwanza na watu **257,825** sawa asilimia **70** walipatiwa chanjo hiyo kwa awamu ya pili katika shehia 33 ambazo huripotiwa kuwa na visa vingi vya wagonjwa wa kuharisha.

### Uratibu wa Shughuli za Kinga Udhibiti wa Maradhi ya Miripuko na Ufuatiliaji wa Maradhi

31. **Mheshimiwa Spika,** ufuatiliaji wa mwenendo wa maradhi umeonesha kwamba magonjwa manne ndio yanayoongoza kwa kuwa na wagonjwa wengi hapa nchini. Magonjwa hayo ni kuharisha (**42,022**), magonjwa ya mfumo wa hewa (**27,519**), tetekuwanga (**22,158**) na waliotafunwa na mbwa (**192**).

32. **Mheshimiwa Spika,** matukio mawili ya kula kasa waliosadikiwa kuwa na sumu yaliripotiwa katika wilaya ya Kaskazini A kwa Unguja na Micheweni kwa Pemba. Jumla ya watu **147** (Unguja **86** na Pemba **61**) waliripotiwa kula kasa huyo na kusababisha vifo vya watu **11** (Unguja **7** na Pemba **4**). Aidha, katika ajali ya boti iliyokuwa na abiria **40** wananchi **10** walipoteza maisha, **25** waliokolewa na watano hawakuonekana.

33. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea na kukabiliana na mripuko wa UVIKO 19 ambapo hadi kufikia Machi 2022, jumla ya washukiwa **1,959** (**1,704 Unguja na 255 Pemba**) na jumla ya watu **142** (**113 Unguja na 29 Pemba**) waligundulika kupata maabukizi ya ugonjwa huu pamoja na vifo **37** (**31 Unguja na 6 Pemba**). Vilevile, jumla wasafiri **174,399** wamefanyiwa vipimo vya UVIKO-19, kati yao wasafiri wasafiri **568** sawa na asilimia **0.32** walibainika kuwa na maaambukizi ya virusi vya UVIKO-19.

**Huduma za Maradhi Yasiyoambukiza**

34. **Mheshimiwa Spika, ,** kitengo cha maradhi yasiombukiza kimekuwa kikisimamia shughuli zote zinazohusiana na maradhi yasiyoambukiza, magonjwa ya Moyo, Kisukari, Saratani, magonjwa sugu ya njia za hewa, Afya ya meno na ajali. Huduma hizi zilitengewa shilingi **737,955,000**. Hadi kufikia Machi, 2022 shilingi **494,923,000** sawa na asilimia **67.1** zilipatikana na kutumika. Katika kuimarisha uchunguzi na matibabu ya maradhi yasiyoambukiza, Wizara imetoa mafunzo ya ugunduzi na matibabu kwa wahudumu wa afya **20** kutoka vituo vya afya **11** na hospitali za Wilaya mbili. Vituo vilivyofikiwa ni Donge Vijibweni, Bumbwini

Misufini, Mahonda, Selemu, Kianga, Polisi Ziwani, JKU, Sebleni, Mpendae, Magirisi na Chuini pamoja na hospitali za Makunduchi na Kivunge. Mafunzo mengine yalitolewa kwa wafanyakazi **60** wa vituo vya afya katika Mkoa wa Mjini Magharibi kwa mashirikiano na Jumuiya ya ZNCD.

35. **Mheshimiwa Spika,** mafunzo ya siku tatu ya utambuzi na kudhibiti shinikizo la damu na athari zake kwa mama wajawazito yalitolewa kwa wahudumu wa vituo vya afya **53**. Lengo ni kupunguza changamoto za mama wajawazito wenye Shinikizo la juu la damu kwa kuwapatia matibabu mapema na kuwapatia rufaa. Aidha, Wizara ilitoa mafunzo ya siku mbili ya uchunguzi wa athari za ugonjwa wa kisukari kwa kutumia "Doppler machine"; ambapo wafanyakazi wanane (8) wa hospitali ya Mnazi Mmoja walishiriki. Baada ya mafunzo hayo wagonjwa **27** wamefanyiwa uchunguzi.

36. **Mheshimiwa Spika,** katika kuongeza uelewa katika ngazi za jamii kuhusiana na maradhi yasioambukiza na vichocheo vyake kupitia vyombo vya habari tofauti vya Serikali na binafsi na kushiriki katika matamasha**.** Wizara ilifanya uchunguzi wa maradhi yasiyoambukiza katika matamasha tofauti tofauti ya Zanzibar. Jumla ya **watu 845** walichunguzwa maradhi yasiyoambukizwa kama vile; kisukari, shindikizo la damu na BMI katika matamasha tafouti siku ya uzinduzi wa Taasi ya Maisha bora, siku ya wanawake duniani na siku ya Umoja wa vijana wa CCM na siku ya kisukari duniani. Aidha matokeo yanaonesha kuwa **asilimia 14** wamekutwa na magonjwa tofauti ya kuambukiza ikiwemo presha na sukari.

**Huduma za Maradhi Yasiyopewa Kipaumbele**

37. **Mheshimiwa Spika,** magonjwa yasiyopewa kipaumbele yamekuwa yakiathiri sana jamii ya wazanzibari. Kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 wagonjwa **5,372** (Unguja **2,493** na Pemba **2,879**) waliogunduliwa namatatizo mbali mbali yakijumuisha minyoo (**4,462)**, matende (**54),** mabusha (**197)**, kichaa cha mbwa (**31)** na kichocho (**514).** Wote waliobainika walipatiwa matibabu stahiki katika vituo vya afya Unguja na Pemba.

38. **Mheshimiwa Spika,** jjumla ya watu 1,190,315 (Unguja 801,715 na Pemba 388,600) kati ya 1,477,054 sawa na asilimia 80 waliweza kufikiwa na kupatiwa dawa za kupambana na maradhi ya minyoo, matende na kichocho katika wilaya zote za Unguja na Pemba. Aidha, jumla ya skuli 860 (Unguja 377 na Pemba 483) zilifikiwa kwa kupatiwa dawa hizo.

**Huduma za Lishe**

39. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ilitoa matone ya Vitamin "A" na upimaji wa hali ya lishe kwa watoto kuanzia umri ya miezi sita hadi miezi 59. Katika zoezi hilo watoto **238,507** kati ya watoto **245,898** (Unguja **166,313,** Pemba **79,585**) sawa na asilimia **97** walifikiwa. Aidha, watoto **36** waligunduliwa na utapiamlo mkali na watoto **856** waligunduliwa na utapiamlo wa kati, wote hao walipatiwa huduma stahiki.

**Huduma za Msingi za Matibabu ya Macho**

40. **Mheshimiwa Spika,** katika utoaji wa huduma za uchunguzi wa macho vijiji **27** vilifikiwa na jumla ya

wananchi **16,763** (wanaume **6,491** na wanawake **10,272)** walichunguzwa**.** Kwa upande wa uchunguzi wa wanafunzi jumla ya skuli kumi zilifikiwa ambapo wanafunzi **13,092** (wanaume **7,157** na wanawake ni **5,935)** walifikiwa**.** Katika uchunguzi huo wanafunzi **105** waligundulika na matatizo ya uhakiki mbaya wa nuru machoni "Refractive Errors" na wanafunzi tisa (**9)** waligundulika na shida ya usikivu. Katika hatua nyengine, wananchi **103** walifanyiwa upasuaji wa mtoto wa macho katika hospitali ya Abdalla Mzee Pemba.

**Huduma za Utoaji wa Elimu ya Afya**

**41. Mheshimiwa Spika,** skuli **35** (Unguja **20 -** Pemba **15**) zimefikiwa na wanafunzi **62,060** walipatiwa elimu ya afya na utunzaji mazingira ili kuwafanya wanafunzi wawe chachu ya mabadiliko katika kinga juu ya maradhi yanayo ambukiza na yasiyoambukiza katika ngazi ya familia na jamii. Vile vile, katika muendelezo wa kutoa elimu ya afya shehia 14 za Pemba zimefikiwa pia kitengo kinaendelea kukutana na masheha ili kuwajengea uwezo kuhusu uelimishaji wa chanjo ya UVIKO 19. Aidha, elimu ya imetolewa katika matamasha mbali mbali yanayofanyika nchini zimefikiwa.

**41. Mheshimiwa Spika,** kupitia kitengo cha elimu ya afya, wizara imeendelea kuwapatia mafunzo wahudumu wa afya wa kujitolea (CHVs) ili waweze kutekeleza kazi zao kwa ufanisi zaidi. Jumla ya wahudumu **220** wamepatiwa mafunzo hayo katika wilaya **11** za Zanzibar; ambapo kila Wilaya ilitoa washiriki 20.

42. **Mheshimiwa Spika,** wahudumu wa afya wamekuwa wakiisaidia wizara katika kuimarisha huduma za elimu ya kinga ili kuweza kuibua, kufuatilia na kuripoti wenye matatizo mbalimbali ya afya. Aidha napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru wahudumu wa afya wa kujitolea kwa kazi kubwa wanayoifanya.

43. **Mheshimiwa Spika**, katika uboreshaji wa huduma za utoaji wa Elimu ya Afya, kitengo cha Elimu ya Afya kimeanzisha 'call center' zitakazotumika na wananchi katika kuripoti na kupata elimu namatukio ya kiafya.Wananchi kupitia 'center' hizo watapata fursa ya kuuliza maswali ya afya na kupatiwa majibu ya papo hapo..

**Huduma za Afya ya Mazingira**

44. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya afya katika kuhakikisha kuwa jamii inapata uelewa wa udhibiti taka ngumu imefanya uhamasishaji kwa wanajamii kutoka shehia 64 za wilaya Mjini, Magharibi A na Magharibi B. Vile vile jumla ya vikundi saba (7) kutoka shehia hizo vilipatiwa mafunzo ya kusarifu taka ngumu mkoani Mwanza kwa lengo la kujifunza kwa wenzetu jinsi wanavyotunza mazingira safi ili kuweza kukabiliana na maradhi ya mripuko kama kuharisha.

45. **Mheshimiwa Spika,** ukaguzi wa vyakula na maeneo mengine ya kijamii ulifanyika kwa Unguja na Pemba kwa lengo la kuangalia usafi na usalama wa chakula na mazingira, nia ni kuikinga jamii dhidi ya maradhi ya kuambukiza. Baadhi ya wafanyabiashara walibainika na makosa ya kutokupima afya zao (medical checkup), uuzaji

wa biashara katika mazingira yasioridhisha, kutokuvaa sare (uniform) muda wa kazi, kutokuwepo sehemu ya kunawia mikono (maji tiririka na sabuni) sambamba na kutokufuata miongozo na kanuni za afya. Wafanyabiashara hao walielekezwa juu ya umuhimu wa kutunza usafi wa maeneo ya biashara za vyakula.

**Huduma za Afya Bandarini**

46. **Mheshimiwa Spika,** jumla ya wageni **328,046** waliingia nchini kupitia bandarini na uwanja wa ndege (bandarini **145,312** na Uwanja wa ndege **182,734**). Wageni wote walifanyiwa ukaguzi wa kiafya, ambapo wageni **29** walishukiwa kuwa na dalili za ugonjwa wa UVIKO-19 na waliripotiwa kwa maafisa ufuatiliaji wa maradhi waliopo wilayani. Aidha, wageni **11** waliogundulika na UVIKO 19 waliripotiwa kwenye vituo vya afya kwa matibabu stahiki.

47. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Afya ikishirikana na kampuni ya Zan Medical imefanya vipimo vya UVIKO 19 kwa wasafiri **93,411** kati yaowasafiri **175** sawa na asilimia**0.19** waligunduliwa na ugonjwa wa UVIKO-19. Aidha, wasafiri **1,124** walipatiwa chanjo za wasafiri, kiwango cha uchanjaji kwa wasafiri kimeongezeka kwa asilimia 73 ukilinganisha na idadi ya wasafiri **824** waliochanjwa mwaka 2020. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo imefanikiwa kutengeneza muongozo wa ukaguzi kwa wasafiri na kutengeneza mfumo wa kujaza fomu ya ufuatiliaji wa magonjwa kwa wasafiri wakiwa nje ya nchi (Online Travelers Surveillance Platform) hatua hii itapunguza kwa kiasi kikubwa msongamano wa abiria mipakani.

### Huduma za Afya ya Wafanyakazi

48. **Mheshimiwa Spika,** wafanyakazi **5,454** walifanyiwa uchungzi wa afya, kati yao **267** sawa na asilimia **4.9** waligunduliwa na matatizo mbali mbali ya afya. Wote walioonekana na matatizo ya afya wamepelekwa kwa daktari kwa uchunguzi zaidi na kupatiwa matibabu sahihi.

### Huduma za Afya ya Msingi ya Akili

49. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea kutowa huduma za afya ya akili katika hospitali zote za wilaya pamoja na Vituo vya daraja la pili ambapo zaidi ya wagonjwa 4000 wanapatiwa huduma nje ya hospital ya Kidongo chekundu. Vile vile elimu ya Afya ilitolewa katika skuli 15 ambapo Zaidi ya wanafunzi 1,789 (1,709 wanawake 710 wanaume ) na walimu 44 walifikiwa. Katika maadhimisho ya siku ya Afya ya akili yaliyofanyika tarehe 1 hadi tarehe 10 Oktoba, 2021 pamoja na kazi nyingine wateja 400 walipatiwa huduma za Afya akili kwenye viwanja vya Kisonge.

50. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha huduma za afya ya akili kwa jamii mafunzo ya siku tano (5) yalitolewa kwa wasimamizi wa wahudumu wa kujitolea - "Community Health Volunteers" zaidi ya **160** kwa lengo la kufuatilia kazi wilayani pamoja na kupata uelewa wa Tiba ya Kuondosha Tatizo itolewayo kwa watu ama wagonjwa wanao sumbuliwa na sonona/msongo wa mawazo na wasiwasi.

51. **Mheshimiwa Spika,** huduma za afya ya akili zimekuwa zikitolewa kupitia huduma maalumu za Afya ya Akili Vijijini ambapo timu ya wataalamu hufika kwenye Shehia husika kwa kutowa huduma kwa siku nzima katika kipindi husika. Jumla ya

Shehia 38 kwenye Vituo 18 zilifaidika na huduma hii ambapo wananchi wasiopungua 3,500 walifaidika na huduma za uchunguzi wa afya ya akili pamoja na kupatiwa huduma nyinginezo.

52. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea na kukabiliana na mripuko wa UVIKO 19 ambapo hadi kufikia Machi 2022, jumla ya washukiwa **1,959** (**1,704 Unguja na 255 Pemba**) na jumla ya watu **142** (**113 Unguja na 29 Pemba**) waligundulika kupata maabukizi ya ugonjwa huu pamoja na vifo **37** (**31 Unguja na 6 Pemba**). Vilevile, jumla wasafiri **174,399** wamefanyiwa vipimo vya UVIKO-19, kati yao wasafiri wasafiri **568** sawa na asilimia **0.32** walibainika kuwa na maaambukizi ya virusi vya UVIKO-19.

53. **Mheshimiwa Spika,** jumla ya wageni **328,046** waliingia nchini kupitia bandarini na uwanja wa ndege (bandarini **145,312** na Uwanja wa ndege **182,734**). Wageni wote walifanyiwa ukaguzi wa kiafya, ambapo wageni **29** walishukiwa kuwa na dalili za ugonjwa wa UVIKO-19 na waliripotiwa kwa maafisa ufuatiliaji wa maradhi waliopo wilayani. Aidha, wageni **11** waliogundulika na UVIKO 19 waliripotiwa kwenye vituo vya afya kwa matibabu stahiki.

54. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Afya ikishirikana na kampuni ya Zan Medical imefanya vipimo vya UVIKO 19 kwa wasafiri **93,411** kati yao wasafiri **175** sawa na asilimia **0.19** waligunduliwa na ugonjwa wa UVIKO-19. Aidha, wasafiri **1,124** walipatiwa chanjo za wasafiri, kiwango cha uchanjaji kwa wasafiri kimeongezeka kwa asilimia 73 ukilinganisha na idadi ya wasafiri **824** waliochanjwa mwaka 2020. Aidha,

Wizara kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo imefanikiwa kutengeneza muongozo wa ukaguzi kwa wasafiri na kutengeneza mfumo wa kujaza fomu ya ufuatiliaji wa magonjwa kwa wasafiri wakiwa nje ya nchi (Online Travelers Surveillance Platform) hatua hii itapunguza kwa kiasi kikubwa msongamano waabiria mipakani.

**PROGRAMU YA TIBA (PH0302)**

55. **Mheshimiwa Spika,** progamu hii ina husika na kusimamia utoaji wa huduma katika hospitali za Mkoa na Wilaya, Aidha, inahusika na huduma za Mpango wa Damu salama, Ushauri kwa Hospitali Binafsi, uchunguzi wa maradhi na kusimamia uendeshaji wa shughuli za mabaraza ya kitaaluma (madaktari, wauguzi na maabara) na huduma za Mkono kwa Mkono.

56. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, kiasi cha shilingi **123,205,936,000** sawa na asilimia 62 ya fedha zote zilizotegwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Wizara. Hadi kufikia machi 2022 Programu hii iliingiziwa kiasi cha shilingi **25,022,753,965** sawa na asilimia kumi na nne (**20.3%)** ya fedha zilizotengwa. Huduma zifuatazo zinatolewa kupitia program ndogo ya huduma za matibabu na huduma za uchunguzi.

**Programu Ndogo ya Huduma za Matibabu (SH030201)**

57. **Mheshimiwa Spika,** huduma hii ilipangiwa kutumia shilingi **116,994,910,000** hadi kufikia Machi, 2022 iliingiziwa kiasi cha shilingi **23,430,980,857** sawa na asilimia 20.

58. **Mheshimiwa Spika,** mahudhurio ya huduma za kliniki maalum yamepungua kutoka **471,754** mwaka 2019/2020, **293,734** ya mwaka 2020/2021 na kufikia **157,224** mwaka 2021/2022**,** huduma hizo zinajumuisha za maradhi ya kisukari, presha, meno na mengine. **Mheshimiwa Spika,** wizara imeingia mkataba na hospitali za Tanzania bara kwa ajili ya kuwapatia wananchi wetu huduma za rufaa. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2022 jumla ya wagonjwa 455 walipelekwa katika hospitali hizo kupata matibabu (MOI 87, Muhimbili National Hospital 131, JKCI 96, ORBIT 105, Ocean Road 36).

59. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyengine, wizara ilipanga kutumia shilingi **920,000,000** kwa ajili ya kusafirisha wagonjwa Tanzania Bara.Hadi kufikia Machi 2022 deni lilikuwa shilingi **2,220,076,913** na Wizara ilifanikiwa kulipa kiasi cha shilingi **1,200,000,000** kwa ajili ya matibabu ya wagonjwa Tanzania Bara.

**Huduma za Damu Salama**

60. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imekusanya uniti za damu **12,252** kutoka kwa wachangiaji wa hiari kwa kipindi cha Julai,2021 - Machi, 2022. Hii ni sawa na asilimia 77 ambapo lengo lilopangwa ni kukusanya uniti 16,000 za damu. Huduma ya damu ni muhimu kwa matumizi ya wagonjwa na mama wajawazito hasa wakati wa kujifungua. Jumla ya uniti **13,937** zilisambazwa katika hospitali kwa matumizi hayo. Ukusanyaji huu ulifanikishwa kupitia mabonanza ya uchangiaji damu yaliyoendelea kufanyika katika maeneo mbali mbali.

**Huduma za Mabaraza ya Kitaaluma**

61. **Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Ushauri wa Hospitali Binafsi, moja ya kazi yake kubwa ni kufanya ukaguzi wa vituo na hospitali binafsi ili kuona vigezo vilivyowekwa vinatimizwa na kufuatwa kwa mujibu washeria nambari 4 ya mwaka 1994. Bodi hiyo ilifanya ukaguzi katika hospitali na vituo vya afya vya binafsi **64** sawa na asilima **67.4** ya vituo **95** vilivyopangwa kukaguliwa. Jumla ya vituo vyote binafsi kwa sasa ni 155.

62. **Mheshimiwa Spika,** mpaka kufikia machi 2022, Vituo 12 vilisimamishwa kutoa huduma kutokana na kasoro zilizogundulika; vituo hivyo ni Glory Clinic, Tamsef dispensary, Azhar Dispensary, Modern Dispensary, Koani Dispensary, Nuru Dispensary, Nyango Dispensary, Hakam Token Clinic, Mustafa Unal Dispensary, Tomondo Dispensary, Sahal Dispensary na Coastal Dispensary. Vituo 10 kati ya vilivyofungiwa kwa sasa vinaendelea kutoa huduma baada ya kufanya marekebisho waliyopewa na vituo 2 vimeshindwa kabisa kuendelea na huduma huduma (Costal na Tomondo Dispensary). Aidha, jumla ya maombi 16 ya kufungua vituo vipya yamepokelewa na kupatiwa usajili baada ya kukidhi vigezo.

**Huduma ya Upatikanaji, Uhifadhi na Usambazaji wa Dawa na Vifaa vya utibabu**

63. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ilitenga jumla ya shilingi **21,209,508,000** kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa vya utibabu, hadi kufika Machi 2022 jumla ya shilingi

**8,756,022,690** zilipatikana sawa na asilimia 41, kati ya hizo shilingi **553,869,890** kutoka kwa washirika wa maendeleo na shilingi **8,202,152,800** kutoka Serikalini.

**Huduma za Tiba Asili na Tiba Mbadala**

64. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hiki cha utekelezaji, Baraza limesajili klinik za Tiba asili **43**, Klinik za Tiba Mbadala 5, Maduka ya dawa asili **179**, Waganga wa tiba asili **165**, wasaidizi waganga **165** pamoja na ghala mbili (2). Aidha, jamii imeelimishwa juu ya matumizi sahihi ya tiba asili na tiba m'badala kupitia vyombo vya habari ambapo wananchi walipata fursa ya kuuliza maswali kwa watendaji wa Baraza hili juu ya tiba hizi.

65. **Mheshimiwa Spika,** kwa muda mrefu, shughuli za Baraza hili zimekuwa zikitatizika kutokana na kutokuwepo kwa usafiri wa uhakika. Ni faraja kubwa kwa sasa, kwani usafiri wa uhakika umepatikana na kazi za ukaguzi zimefanyika. Kwa kushirikiana na jeshi la Polisi, Baraza limefanikiwa kumkamata mtabibu mmoja wa dawa za asili ambae amekiuka miongozo ya tiba hizi. Kutokana na kazi hizi za ukaguzi, wimbi kubwa la wanaojilabu na kutoa matangazo ya tiba asili kwenye vyombo vya habari kinyume na sheria limepungua. Kwa upande mwengine, Baraza limefanya utafiti wa mimea ya dawa inayopatikana katika mkoa wa kusini Unguja na ripoti ya utafiti huo ipo tayari. Aidha, vibali **98** vya kusafirisha dawa nje ya nchi (Export Permit) vimetolewa na kwa upande wa uingizaji dawa nchini vibali vitatu (3) vilitolewa.

**Programu Ndogo Huduma za Uchunguzi (SH030202)**

66. **Mheshimiwa Spika,** huduma hii ilipangiwa kutumia shilingi **6,231,026,000,** hadi kufikia Machi, 2022 iliingiziwa kiasi cha shilingi **1,591,863,108** sawa na asilimia 26.

**Huduma za Chakula, Dawa na Vipodozi**

67. **Mheshimiwa Spika,** katika kazi zake za kawaida, Wakala wa Chakula na Dawa imefanya ukaguzi wa maeneo ya biashara **3,252** kati ya **3,534** sawa na asilimia (92). Ukaguzi huo umejumuisha maeneo ya chakula **2,300**, dawa **724**, vipodozi **198** na vifaa tiba **30**. Katika ukaguzi huo maeneo **15** ya kuuzia dawa yalizuiliwa kuendelea na biashara kutokana na kutokidhi vigezo vilivyowekwa yakiwemo maduka makubwa ya dawa sita (6) na maduka madogo ya dawa tisa (9). Aidha, tani **200.5** (chakula **178**, dawa **18** na vipodozi **4.5**) zisizofaa kwa matumizi ya binadamu ziliteketezwa ambapo tani **260** za mchele zimerudishwa sehemu zilikotoka kwa mujibu wa Sheria.

68. **Mheshimiwa Spika,** Taasisi imesajili maeneo **847** (chakula **436**, dawa **363**, vipodozi **31** na vifaa tiba **17**) ni sawa na asilimia (75) ya shabaha iliyowekwa ya kusajili maeneo **1,132** ya biashara/uzalishaji wa bidhaa. Kwa upande wa bidhaa, jumla ya maombi **244** (Chakula **75**, dawa **3**, vipodozi **164** na **2** za vifaa tiba) yalisajiliwa baada ya kufanyiwa tathmini na kukidhi vigezo vilivyowekwa. Aidha, sampuli **1,879** za Chakula **1,646**, Dawa **73**, Vipodozi **139** na vifaa tiba **21** zilifanyiwa uchunguzi, kati ya hizo sampuli **242** (Chakula **239**, vipodozi 1, vifaa tiba 2) hazikufikia viwango.

**Huduma za Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali**

69. **Mhesimiwa Spika,** Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imefanikiwa kuchunguza jumla ya sampuli **585** (Unguja **558** na Pemba **27**) zikiwemo sampuli **25** za vinasaba. Katika hatua nyengine, vibali **729** (Unguja **541** na Pemba **188**) vya uingizwaji na utoaji wa kemikali vilitolewa sambamba na kusajili majengo **16** ya uhifadhi wa kemikali. Vile vile, maeneo **18** yalifanyiwa ukaguzi (Unguja **15** na Pemba **3**). Maabara pia iliwapatia mafunzo ya GC - MS watendaji wawili wa maabara.

**PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA (PH0305)**

70. **Mheshimiwa Spika,** programu hii inahusika na usimamizi wa rasilimali watu, rasilimali fedha, manunuzi, sheria na shughuli nyengine za uendeshaji wa Wizara. Aidha, ina jukumu la kuandaa na kusimamia sera, miongozo, mipango pamoja na kuratibu taarifa za afya.

**Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji (SH030501)**

71. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ilipangiwa kutumia kiasi cha shilingi **8,335,051,000** na hadi kufikia Machi 2022 iliingiziwa jumla ya shilingi **4,477,593,281** sawa na asilimia 53.7.

72. **Mheshimiwa Spika,** kwa kushirikiana na Taasisi ya Benjamin Mkapa, Wizara imeajiri wafanyakazi **105** wa mkataba wakiwemo maafisa tabibu (**43**), wauguzi (**57**), wataalamu wa maabara (**13**) maafisa afya ya mazingira (**10**), wataalmu wa mionzi na picha wawili (**2**), na wahudumu (**10**). Aidha, wafanyakazi **20** wameajiriwa na kupelekwa katika hospitali

ya Wagonjwa wa Akili Kidongo Chekundu. Katika hatua nyengine, wafanyakazi **143** wamemaliza masomo ya kada mbali mbali wakiwemo wataalamu wa mionzi wanne (**4**), wataalamu wa ngozi wawili (**2**), mtaalamu wa magonjwa ya watoto mmoja (**1**), na mtaalamu wa uchunguzi wa maradhi mmoja (**1)**.

73. **Mheshimiwa Spika,** jumala ya wafanyakazi ambao wapo masomoni ni **595** katika vyuo tofauti vya ndani na nje ya Tanzania, kati ya hao 353 wanasoma ndani ya Tanzania na 242 wanasoma nje ya Tanzania kwa kada tofauti. Pia wizara imekamilisha kuandaa muongozo wa mafunzo kwa lengo la kupanga na kufanya ufuatiliaji wa mafunzo kwa watendaji wa afya. Kuwepo kwa muongozo huu kutasaidia kutoa fursa sawa za mafunzo kwa watendaji sambamba na kupunguza tatizo la wafanyakazi wengi kwenda masomoni kunakosababisha upungufu wa watendaji katika hospitali na vituo vya afya na hivyo kuzorotesha utoaji wa huduma.

74. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kwamba utendaji kazi unafuata kanuni na taratibu zilizowekwa, Wizara imetiliana saini makubaliano na taasisi mbali mbali katika utekelezaji wa majukumu yake. Jumla ya mikataba **67** imetayarishwa ikiwemo mikataba ya ujenzi wa hospitali **10** za wilaya na hospitali moja ya mkoa yenye thamani ya shilingi bilioni **60.**

75. **Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza Mkakati wa Dijitali ya Afya, ambapo Wizara inaendelea na kutengeneza mfumo wa usajili wa wagonjwa ("Client Registry"), mfumo wa kukusanya taarifa za maradhi ya mripuko

(eIDSR), mfumo wa kusajili dawa na vifaa tiba ("Zanzibar Health Commodities Catalogue", mfumo wa kuweka taarifa za wagonjwa ("Electronic Medical Record Readiness Assessment") na "Digital Health Blue Print". Mifumo hii inategemewa kukamilika mwishoni mwa Juni, 2022 na kuanza kutumika mwaka wa fedha 2022/2023.

76. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyengine Wizara inaendelea na utengenezaji wa mfumo wa "Insurance Management Information System" ambao unategemewa kutumika sambamba na maamuzi ya Serikali ya kutekeleza Bima ya Afya kwa wote. Mfumo huo unategemewa kukamilika mwezi wa Julai na kuanza kutumika rasmi mwezi wa Agosti 2022.

77. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeunda Kamati mpya ya Ukaguzi ambayo ilizinduliwa rasmi na Katibu Mkuu wa Wizara. Tokea kuanzishwa kwake Kamati imefanya vikao vitatu na kufanya mapitio ya ripoti mbali mbali za ukaguzi zikiwemo ripoti ya ukaguzi wa ndani kwa mwaka 2020/2021. Maelekezo juu ya mapungufu yaliyobainika yalitolewa kwa wahusika wote walioguswa na taarifa ya utekelezaji wake imeandaliwa.

**Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti (SH030502)**

78. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 programu hii ilitengewa kiasi cha shilingi **3,738,164,000**, hadi kufika Machi iliingiziwa shilingi **481,905,950** zaidi ya asilimia 13**.**

79. **Mheshimiwa Spika,** ili kufikia azma ya Serikali ya kuanzisha bima ya afya hatua mbali mbali zimefikiwa ikiwemo kukamilika kwa usarifu wa awali wa mfuko wa huduma za afya, kukusanywa maoni ya wananchi juu ya usarifu wa mfuko wa huduma za afya, kukamilika kwa usarifu wa awali wa kitambulisho cha wanachama, fomu za usajili na nembo ya mfuko na kukamilika kwa mapitio ya sheria mbali mbali kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa mfuko.

80. **Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Wizara umekamilika na umeanza kutumika. Vile vile, Wizara imetayarisha taarifa mbali mbali za utekelezaji wa Wizara zikiwemo za mwaka na robo mwaka; taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo; na taarifa za Kamati za Baraza la Wawakilishi, ripoti ya utekelezaji wa Wizara kwa mwaka 2020/2021 pamoja na Hotuba ya Bajeti ya mwaka 2022/ 2023, ambayo leo ninaisoma mbele ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. . Taarifa nyengine zilizotayarishwa ni utekelezaji wa ilani na maagizo mbali mbali ya serikali, taarifa ya maendeleo ya sekta ya afya katika maadhimisho ya miaka 58 ya Mapinduzi ya Zanzibar na taarifa ya Wizara ya Afya katika hotuba ya Makamo wa Pili wa Rais.

81. **Mheshimiwa Spika,** mipango na miongozo mbali mbali imetayarishwa ikijumuisha muongozo wa rufaa katika ngazi ya afya ya msingi, ngazi ya afya ya kati na ngazi ya rufaa, pamoja na Mpango Mkakati wa Taarifa za Afya. Aidha, Wizara imeanza kazi ya kufanya mapitio ya sera ya afya ya mwaka 2011 ambapo kwa sasa ripoti ya hali halisi ya utekelezaji wa sera hii imekamilika. Hatua inayofuata

kwa sasa ni kutayarisha sera yenyewe ambayo inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Juni, 2022.

**Taasisi ya Utafiti wa Afya**

**82. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Taasisi hii ilipangiwa kiasi cha shilingi **975,672,000,** hadi kufikia Machi 2022 shilingi **160,445,345** sawa na asilimia 16 zilipatikana.

**81. Mheshimiwa Spika,** Taasisi ya Utafiti wa Afya imekamilisha utafiti wa kujua kinga katika miili ya wakaazi wa Zanzibar mara baada ya ugonjwa wa Korona**.** Vile vile, inaendelea na utafiti wa ongezeko la thamani kwa dawa za miti shamba kwa kutibu maradhi yasiyoambukiza Zanzibar (value addition for herbal medicine used for managing of non-c o m m u n i c a b l e diseases in Zanzibar).

**Programu ndogo ya Uratibu wa Wizara ya Afya Pemba (SH030503)**

**83. Mheshimiwa Spika,** programu hii ilitengewa shilingi **13,513,232,000,** hadi kufikia Machi, 2022 jumla ya shilingi **10,174,645,593** sawa na asilimia 75.3 ziliingizwa.

**84. Mheshimiwa Spika,** programu hii inahusika na uratibu wa shughuli zote za afya kwa upande wa Pemba. Kupitia programu hii hospitali ya Chake Chake imefanyiwa matengenezo ya chumba cha upasuaji mkubwa pamoja na kuwekewa taa mpya na “saction machine” mbili. Vile vile, kinu cha kuchomea taka kimefanyiwa matengenezo sambamba. Aidha, katika hospitali ya Wete kumefanyika matengenezo ya miundombinu ya maji.

**PROGRAMU YA HOSPITALI YA MNAZI MMOJA (H02)**

85. **Mheshimiwa Spika,** shughuli za Programu hii zinatekelezwa kupitia programu ndogo mbili (2); ambazo ni programu ya huduma za uchunguzi na matibabu; na programu ya uongozi na utawala wa hospitali. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 wizara ilitenga jumla ya **shilingi 20,371,200,000** ambapo hadi kufikia Machi, 2022 shilingi **12,398,722,600** sawa na asilimia **61** ziliingizwa kwa ajili ya utekelezaji. Utekelezaji wa programu hizi unafafanuliwa kama ifuatavyo: -

**Programu Ndogo ya Uchunguzi na Matibabu (SH0201)**

86. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hiki cha utekelezaji, wizara kupitia programu hii ilitengewa jumla ya shilingi **813,382,000** ambapo hadi kufikia Machi, 2022 jumla ya shilingi **650,724,000** sawa na asilimia **80** ziliingizwa kwa ajili ya utekelezaji. Jumla ya vipimo vya maabara **159,587** na vipimo **38,222** kwa njia ya picha (Ultrasound ni **16,810**; X-ray **15,114**; MRI **1,316**; na CT Scan **4,982**) vilifanyika katika Hospitaliya Mnazi Mmoja.

87. **Mheshimiwa Spika,** huduma za matibabu zimeendelea kutolewa ambapo mahudhurio ya wagonjwa waliopatiwa matibabu ya nje wamepungua kutoka **107,557** kwa kipindi cha Julai,2020 Machi,2021 kufikia wagonjwa **74,639** wakiwemo wagonjwa **69,029** walihudhuria katika kliniki za magonjwa maaalum**.**

88. **Mheshimiwa Spika,** wagonjwa **14,679** (wanawake **7,515** na wanaume **7,164**) walilazwa kwa magonjwa tofauti, kati yao

wagonjwa **546** walilazwa kwa matatizo ya akili katika hospitali ya Kidongo Chekundu. Aidha, wajawazito **13,385** walilazwa katika Hospitali ya Mwembeladu na Mnazi Mmoja ambapo wajawazito **12,117** walijifungua ambapo wajawazito **2,138 (**asilimia 17) walijifungua kwa njia ya upasuaji.

**89.** **Mheshimiwa Spika,** huduma za matibabu ya kusafisha damu (dialysis) kwa wagonjwa wenye matatizo ya figo zimeendelea kutolewa kwa wagonjwa **371** wakiwemo wa marudio. Aidha, mahudhurio ya wagonjwa **1,714** yalifanyika katika kliniki ya Saratani kwa ajili ya kupatiwa huduma; saratani ya matiti imeendelea kuongoza kwa kuwa na wagonjwa wapya **37** ikifuatiwa na saratani ya mlango wa kizazi kwa kuwa na wagonjwa **16**. Katika hatua nyengine, mahudhurio ya wagonjwa **3,421** wamepatiwa matibabu katika kliniki maalum ya maradhi ya moyo, ambapo wagonjwa **1,786** ni wapya na wagonjwa **1,635** wa marejeo.

**90.** **Mheshimiwa Spika,** hospitali ya Mnazi Mmoja imeendelea kutoa huduma za upasuaji mkubwa kwa wahitaji mbali mbali. Wagonjwa **1,445** (wanawake **563** na wanaume **563**) walifanyiwa upasuaji mkubwa. Kati ya hao, wagonjwa **266** walifanyiwa upasuaji wa kuondoa hania (Herniotomy) na wagonjwa **159** walifanyiwa upasuaji wa tumbo (Laparatomy). Pia, katika muendelezo wa kutoa huduma hiyo ya upasuaji Hospitali ya Mnazi Mmoja imefanikiwa kufanya upasuaji wa matundutumboni (Laparascopy) kwa wagonjwa watatu **(3)**.

91. **Mheshimiwa Spika,** katika kuwapunguzia wananchi na Serikali gharama za matibabu ya nje ya nchi, hospitali imeendesha kambi za uchunguzi na matibabu kwa mashirikiano na madaktari bingwa kutoka Hispania, wataalamu wa moyo na mifupa kutoka Hospitali ya SIMS ya India na wataalamu wa macho kutoka hospitali ya Benjamin Mkapa ya Dodoma. Jumla ya kambi **10** zilifanyika na wagonjwa **549** walichunguzwa na kupatiwa matibabu. Kati ya hao wagonjwa **177** walifanyiwa upasuaji wakiwemo wagonjwa **118** wenye matatizo ya vichwa maji, matatizo ya mgongo wazi na midomo sungura. Kwa wagonjwa wote hawa zingehitajika fedha za Serikali zaidi zaidi ya bilioni mbili kwa kuwasafirisha nje ya Zanzibar kwa upasuaji. Pia Watoto **22** walifanyiwa upasuaji wa midomo sungura, wagonjwa **37** ni matatizo ya mifupa na watoto **33** wanahitajika kufanyiwa upasuaji wa moyo nje ya Zanzibar.

**Programu Ndogo ya Uongozi na Utawala (SH0202)**

92. **Mheshimiwa Spika,** programu hii ilitengewa kutumia jumla yashilingi **19,557,818,000** ikiwa ni pamoja na mishahara ya wafanyakazi. Hadi kufikia Machi, 2022, jumla ya **shilingi 11,747,998,600** sawa na asilimia **60** zilipatikana.

93. **Mheshimiwa Spika,** jumla ya wafanyakazi **25** wamemaliza masomo ya muda mrefu na kurejea kazini wakiwemo wauguzi wa shahada ya kwanza (**18)**, daktari mmoja (**1)**, muuguzi bingwa wa afya ya akili mmoja (**1)** na madaktari bingwa watano **(5)**. Kati ya madaktari watano (5) wamo wataalamu wa ngozi wawili (**2**), mtaalamu wa magonjwa ya watoto mmoja (**1**), mtaalamu wa rediolojia mmoja (**1**) na mtaalamu wa uchunguzi wa maradhi mmoja (**1)**. Vile vile, wafanyakazi **132** wa hospitali ya Mnazi Mmoja walipatiwa

mafunzo ya muda mfupi yaliyohusisha "Abdominal Ultra-Sound" (**23**), "Emergency Care (**36**), kutumia kifaa kipya cha kusikiliza mapigo ya moyo ya mtoto (**64**) na mafunzo ya "Oxygen Plant" (**9**).

94. **Mheshimiwa Spika,** kama mnavyokumbuka kwamba hivi karibuni hospitali ya Mnazi Mmoja imekamilisha ujenzi wa chumba cha kuhifadhia maiti chenye uwezo wa kuhifadhi maiti 20 kwa wakati mmoja. Sambamba na hilo hospitali kwa sasa imejenga kisima na mitambo miwili ya kusafishia maji chumvi, hivyo kupunguza tatizo la maji katika hospitali hii.

## UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

### Ujenzi wa Maabara ya Uchunguzi ya Chakula, Dawa na Vipodozi

95. **Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa Maabara ya kisasa ya Wakala wa Chakla na Dawa umefikia asilimia 95, takriban ujenzi huo umekamilika hatua inayoendelea sasa ni ufungwaji wa mfumo wa udhibiti wa hewa (Air Handling nit) na milango maalum ya kuzuia maambukizi katika maabara ya Mikrobiolojia (Hermetic Doors). Aidha, mawasiliano na ZECO juu ya kuweka "transformer" maalum kwa ZFDA ili kufanya majaribio na baadae matumizi ya vifaa katika maabara hiyo yameshafanyika.

### Ujenzi wa Maabara ya Uchunguzi wa Virusi - Binguni

96. **Mheshimiwa Spika,** ujenzi wa jengo la maabara ya Microbiology, Phytochemistry na maabara itakayotumika kupima virusi vya COVID-19 umekamilika. Aidha, ujenzi

wa jengo la pili la Utawala limekamilika natayari limeshaanza kufanya kazi. Katika hatua nyengine, mchakato wa ujenzi wa maabara ya Bio-Chemistry umeanza ambapo hatua za awali za kupata michoro na BOQ imeshakamilika kupitia wakala wa Majenzi Zanzibar. Michoro hiyo imeshakabidhiwa kwa Wizara na kazi ya zabuni ya kumtafuta mkandarasi imeanza.

**Utekelezaji wa Miradi ya IMF**

**97. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia fedha za IMF inaendelea na ujenzi wa hospitali 10 za wilaya na hospitali moja (1) ya Mkoa wa Mjini Magharibi. Mpaka kufikia Machi 2022 ujenzi wa hospitali hizi ni kati ya asilimia 50. Kuwepo kwa hospitali hizi kutasaidia sana kufikisha huduma za afya karibu na wananchi pamoja na kuipunguza idadi ya wagonjwa wanaohudhuria hospitali ya rufaa ya Mnazi Mmoja. Hadi kukamilika kwake ujenzi wote unategemewa kutumia kiasi cha shilingi **60,148,111,863.12** na shilingi **21,451,453,290** kwa ajili ya ununuzi wa vifaa, gari za kubebea wagonjwa na gari za kusambazia dawa ambapo hadi Machi 2022 shilingi **24,413,483,411** sawa na asilimia **40.6** zimeshalipwa. Ujenzi wa hospitali za wilaya unatarajiwa kukamilika ifikapo mwisho wa mwezi wa Juni, 2022. Katika kutekeleza miradi hiyo kupitia fedha za IMF Wizara ililazimika kufanya uhaulishaji wa shilingi **69,000,177,740** kutoka katika Miradi ya Maendeleo kati ya shilingi **81,599,563,153.12** zilizopangwa.

**Mradi wa Kupandisha Hadhi Hospitali ya Mnazi Mmoja**

98. **Mheshimiwa Spika,** Mradi huu una lengo la kuimarisha huduma katika hospitali hii ya rufaa ya Mnazi Mmoja kwa kuimarisha miundombinu ya hospitali hiyo ikiwa ni pamoja na kufanya ununuzi wa vifaa mbali mbali vya kisasa vya utibabu. Katika kipindi hichi cha utekelezaji hospitali ilifanya ununuzi wa mashine ya Probe, ununuzi wa vifaa vya ufundi, ununuzi wa viyoyozi pamoja na ununuzi wa komputa.

99. **Mheshimiwa Spika,** hospitali ya Mnazi Mmoja imeingia katika mradi mkubwa wa upanuzi wa hospitali kupitia mradi wa BADEA, "Saudi Fund" na "Kuwait Fund" kwa kufanya shughuli mbali mbali zikiwemo za ujenzi na upanuzi wa majengo pamoja na ununuzi wa vifaa vya utibabu. Timu ya kuratibu Mradi huo (Project Implementation Unit - PIU) tayari imeshachaguliwa na imeanza kazi.

**Ujenzi wa Hospitali ya Wagonjwa wa Akili**

100. **Mheshimiwa Spika**, **35.** ujenzi wa hospitali ya wagonjwa wa akili Kidongo Chekundu uliofadhiliwa kwa pamoja baina ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Haukeland University Hospital ya Norway umekamilika na kufunguliwa rasmi na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt Hussein M w i n y i. Huduma za afya ya akili zimeimarishwa kwa kuongezwa kwa wodi ya huduma za waraibu wa madawa ya kulevya na wodi ya watoto na kuwekwa chumba maalumu cha wagonjwa wa dharura. Mradi huo mpaka kukamilika kwake umegharimu jumla ya shilingi 5,260,412,860.

**Ujenzi wa Hospitali ya Wete**

**101. Mheshimiwa Spika, 35.** ujenzi wa hospitali ya Wete unaotarajiwa kutekelezwa kupitia fedha za ufadhili kutoka Serikali ya Abudhabi, tayari mshauri elekezi ameshapatikana na ujenzi unatarajiwa kuanza mwezi Agosti, 2022. Ujenzi wa Hospital hii unaratibiwa kupitia Mfuko wa Maendeleo wa Abudhabi (Abudhabi Fund for Development).

**Mheshimiwa Spika**, Hospitali hiyo inatarajiwa kuwa ya kisasa yenye vitanda kuanzia 100, itakayotoa huduma za MRI, CT-scan, X rays, huduma za upasuaji, huduma za dialysis, huduma za kisasa za maabara na nyenginezo.

**Ujenzi wa Wodi ya Mama na Mtoto Hospitali ya Chake Chake**

**102. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha huduma za mama na mtoto zinaimarishwa, Wizara inaendelea na ujenzi wa wodi ya mama na mtoto katika hospitali ya Wilaya ya Chake Chake ambao umefikia hatua nzuri ya utekelezaji wake. Mradi huu unatarajiwa kukamilika katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2022/ 2023.

**Ujenzi wa nyumba za Wafanyakazi Hospitali ya Abdalla Mzee**

**103. Mheshimiwa Spika**, nyumba za wafanyakazi katika hospitali ya Abdalla Mzee zitajengwa kwa msaada kutoka Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kwa utaratibu wa kujengea nyumba hizo na kutukabidhi ufunguo baada ya kukamilika (turn key project). Ujenzi umechelewa utekelezaji wake kutokana na kuibuka kwa janga la maradhi ya UVIKO-19 duniani. Wakandarasi wa kichina walikuja nchini na kwa kushirikiana na wizara taratibu zote za ujenzi zimekamilika ikiwa ni pamoja nakupata kibali cha ujenzi na tunatarajia ujenzi huo utaanza muda mfupi ujao.

## MWELEKEO WA BAJETI NA VIPAUMBELE VYA WIZARA KWA MWAKA 2022/2023

**104. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2022/2023, vipaumbele vya wizara vimezingatia mapendekezo yaliyotolewa katika mapitio ya utekelezaji ya Wizara kwa mwaka 2020/2021; Mpango Mkakati wa Nne wa Wizara; Mikakati ya Kitaifa na Kimataifa, Dira ya Maendeleo 2050, Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020/2025 na maagizo ya Serikali. Vipaumbele hivyo vinagusa maeneo yafuatayo: -

i) Kuimarisha Afya ya Uzazi wa Mama na mtoto kupunguza vifo vya mama wajawazito na watoto wachanga
ii) Kuimarisha upatikanaji wa Dawa, vifaa vya utibabu na uchunguzi
iii) Kuanzisha Bima ya Afya
iv) Kuimarisha nguvu kazi ya Afya
v) Kuimarisha huduma za Afya ya Msingi
vi) Kuimarisha uwezo na utayari wa kupambana na maradhi ya mripuko na majanga ya kiafya
vii) Kuendeleza mapambano dhidi ya maradhi ya kuambukiza na yasiyoambukiza
viii) Kuimarisha miundombinu ya utoaji wa huduma za Afya
ix) Kuimarisha matumizi ya taarifa za afya katika kufanya maamuzi

## SHUGHULI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA NA WIZARA YA AFYA KWA MWAKA 2022/2023

**105. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha vipaumbele vilivyoainishwa hapo juu vinafikiwa, Wizara itatekeleza shughuli zilizopangwa kupitia programu husika kama ifuatavyo: -

## PROGRAMU YA KINGA NA ELIMU YA AFYA (PH0101)

106. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/ 2023, Wizara imetenga shilingi **34,418,113,000** sawa na asilimia **22.3** ya bajeti ya Wizara ili kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i) Kuimarisha uwezo na utayari wa kupambana na maradhi ya mripuko na majanga ya kiafya.

ii) Kuongeza uelewa kwa jamii juu ya utekelezaji wa afua zinazolenga kukinga maradhi tofauti yakiwemo ya kumabukiza na yasiyoambukiza

iii) Kuimarisha utoaji wa huduma za afya ya msingi katika Wilaya pamoja na kuboresha huduma za lishe

iv) Kuimarisha huduma za afya ya kinywa na meno pamoja na macho

v) Kuendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma za chanjo ili kudhibiti maradhi yanayozuilika kwa chanjo

vi) Kuimarisha utoaji wa huduma shirikishi za UKIMWI, Kifua Kikuu, Homa ya Ini na Ukoma

vii) Kuimarisha huduma za afya ya Mama na Mtoto ili kupunguza magonjwa na vifo

viii) Kuboresha huduma za afya mipakani ikiwemo bandari na viwanja vya Ndege

ix) Kuimarisha afya ya mazingira.

## PROGRAMU YA TIBA (PH0102)

107. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, programu hii imepangiwa kutumia shilingi **90,410,826,000** sawa na asilimia **58.7** kwa ajili ya kutekeleza shughuli kuu zinazotekelezwa na programu hii. Hivyo, naliomba Baraza hili liidhinishe matumizi kwa ajili ya shughuli zifuatazo:-

i) Kujenga hospitali mpya ya wagonjwa wa akili eneo la Kinyasini Pemba na hospitali ya Mkoa wa Kaskazini Unguja katika eneo la Mahonda
ii) Kujenga kituo cha damu salama Pemba
iii) Ukarabati mkubwa wa hospitali ya Wete
iv) Kuanzisha na kuhakikisha ngazi zote za utoaji wa huduma zinafuata miongozo na viwango vilivyothibitishwa na wizara ya afya katika utoaji wa huduma (national standards).
v) Kuanzisha utaratibu maalum wa utoaji wa huduma za afya kwa watalii
vi) Kuanzisha viwanda vya kutengeneza dawa na vifaa tiba
vii) Kuimarisha usimamizi katika uhifadhi na utumiaji wa dawa na vifaa tiba katika hospitali na vituo vya afya
viii) Ununuzi wa vifaa vya maabara ya Wakala wa Chakula na Dawa
ix) Kuanzisha vyama vya kitaaluma "professional associations" ikiwemo wafamasia, wataalamu wa ubongo na uti wa mgongo, huduma za dharura, magonjwa ya kinamama na watoto, afya ya akili na nyenginezo
x) Kuimarisha mashirikiano na vyuo vikuu vya ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kusimamia miongozo ya utoaji huduma na mafunzo endelevu kwa wafanyakazi
xi) Kubadilisha mfumo wa utoaji wa huduma katika ngazi zote
xii) Kuanzisha '**Center of Excellence for superspecialized medical services'** kwa ajili ya matibabu ya moyo, mifupa na ajali (traumatology), saratani, uti wa mgongo na ubongo, macho na meno na nyenginezo.

**PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA (PH0103)**

108. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023, wizara imepanga kutumia shilingi **29,206,170,000** sawa na asilimia **19.0** ya bajetiya wizara kwa ajili ya shughuli zilizomo katika programu hii. Shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na:-

i) Kuimarisha mashirikiano na sekta binafsi katika utoaji huduma mbali mbali katika hospitali na vitengo ikiwemo huduma za uchunguzi.

ii) Kuanzisha muongozo utakaotumika kutoa madaraja kwa hospitali na vituo vya afya hapa Zanzibar.

iii) Kupima utendaji na uwajibikaji wa wafanyakazi ili kuboresha huduma kwa wateja

iv) Kuweka mfumo wa kutambua mahitaji halisi ya wafanyakazi kwa ngazi tofauti kuanzia hospitali za vijiji, wilaya hadi Mkoa

v) Kuanzisha ‘Succession Plan’ (Urithishwaji kazi baada ya muhusika mkuu kuondoka)

**PROGRAMU YA HOSPITALI YA MNAZI MMOJA (H02)**

109. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 jumla ya shilingi **34,186,349,000** zimepangwa kutumika kwa hospitali ya Mnazi Mmoja. Kati ya hizo shilingi **14,694,200,000** kwa ajili ya mishahara, na shilingi **5,969,930,000** kwa ajili ya shughuli za uendeshaji wa hospitali. Aidha, shilingi **13,522,219,000** zimepangwa kutumika kwa shughuli za maendeleo zikiwemo shilingi **5,553,000,000** kutoka Serikalini na shilingi **7,969,219,000** kutoka kwa washirika wa

maendeleo. Zifuatazo ni shughuli kuu zitakazotekelezwa na hospitali ya Mnazi Mmoja kwa mwaka 2022/2023.

i) Kuendelea kutoa huduma za kibingwa ikiwemo usafishaji damu kwa wagonjwa wa figo, uchunguzi wa saratani (biopsy), matibabu ya satarani (chemotherapy), huduma za ubongo na uti wa mgongo
ii) Kuimarisha upatikanaji wa huduma za uchunguzi kwa wagonjwa pamoja na upatikanaji wa huduma za matibabu ya rufaa
iii) Kuimarisha kitengo cha usimamizi wa tafiti na kuendeleza uwezo wa kufanya tafiti za afya
iv) Kupunguza idadi ya wagonjwa wanaopewa rufaa za nje ya nchi kupitia uimarishaji kambi maalum za matibabu
v) Kununua mtambo wa kuzalisha 'oxygen' (Oxygen Plant)
vi) Kununua mashine kubwa ya kuangamiza taka hatarishi (500Kg. medical waste per day).
vii) Kuimarisha miundo mbinu ya hospitali kwa kufanya ukarabati mkubwa na upanuzi wa hospitali ikiwemo ununuzi wa mashine na samani za kisasa za hospitali pamoja na kuongeza idadi ya wataalam bingwa wakiwemo madaktari na wauguzi
viii) Kuimarisha mfumo wa kielektroniki wa kuhifadhi taarifa za wagonjwa Electronic Medical Record (EMR) kwa kununua kompyuta 200 za ziada pamoja na kuongeza wataalam wa TEHAMA ambao watakuwa wanakaa shift masaa 24 na siku zote saba (7) za wiki.
ix) Kuimarisha huduma za bima na huduma za haraka kwa kufanya ukarabati wa jengo, kuweka vifaa vya kisasa na kuanzisha kliniki baada ya muda wa saa za kazi.

## SHUKRANI

110. **Mheshimiwa Spika,** Wizara hii katika kipindi hiki cha utekelezaji, imepata mafanikio katika maeneo mbali mbali ikiwemo kuimarika kwa miundombinu ya afya ikiwemo kuanza kwa ujenzi wa hospitali za Wilaya na Mkoa, kukamilika hospitali ya wagonjwa wa akili, kukamilika kwa maabara ya upimaji wa Uviko 19 pamoja na maradhi mengine ya miripuko, kukamilika maabara kwa ajili ya huduma za Wakala wa Chakula Dawa na Vipodozi. Aidha, Wizara imepata wafanyakazi wa mkataba kupitia shirika la Mkapa Foundation ambao wanasaidia sana katika utoaji wa huduma za afya, kupatikana kwa vifaa vya kisasa kwa ajili ya utoaji wa elimu ya afya nchini, uwepo wa wafanyakazi wa kujitolea ambao ni chachu katika upatikana wa huduma za mama na mtoto katika ngazi ya jamii. Mafanikio haya yametokana na nguvu za pamoja na mshikamano yaliopo baina ya Wizara na Taasisi nyengine za ndani na nje ya nchi na washirika mbali mbali wanaohusika na masuala ya afya. Nachukuwa fursa hii kuwashukuru wale wote waliochangia mafanikio haya pamoja na wale walioshirikiana na Wizara kwa njia moja au nyengine katika kuunga mkono juhudi za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kuimarisha huduma za afya.

111. **Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee nawashukuru wale wote waliochangia katika kufanikisha kazi hii. Shukrani pekee ziende kwa Naibu Waziri wa Afya Mheshimiwa Hassan Kh. Hafidh. Aidha, nawashukuru watendaji wote wa afya akiwemo Katibu Mkuu Dkt. Fatma H. Mrisho, Mkurugenzi Mipango Sera na Utafiti pamoja na wakurugenzi wengine kwa moyo wa kujituma na uzalendo waliouonyesha.

**112. Mheshimiwa Spika,** shukrani ziende kwa Serikali ya Denmark, Jamhuri ya watu wa China, Serikali ya Cuba, India, Kuwait, Marekani, Saudi Arabia, Abudhabi, Oman, Ujerumani. Aidha, nashukuru mashirika ya Maendeleo, yakiwemo Shirika la Afya Ulimwenguni - WHO, UNICEF, UNFPA, PS3+, PATH, MDH, Swiss Embassy, GIZ, Danida, Haukeland University Hospital ya Norway, Mfuko wa kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria (GFATM); SAVE THE CHILDREN, Engender Health, D -Tree International, World Diabetic Foundation, Sight Saver, HIPZ, JHPIEGO, PharmAccess International, Measure Evaluation, Mfuko wa Rais wa Marekani wa Kupambana na Malaria (PMI), CDC, THPS, DFID, AMREF, WATER AID, PEPFAR, ZOP, UNDP, EAC, Zanzibar Milele Foundation, kundi la G-20. Pia, nawashakuru wale wote ambao sikuweza kuwataja katika orodha hii. Hata hivyo, watambue kwamba michango yao tunaithamini sana.

## HITIMISHO

## MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2022/2023

113. **Mheshimiwa Spika,** nawaomba Wajumbe wa Baraza waipokee taarifa hii ya mapendekeo ya bajeti, waijadili kwa uwazi na hatimae wakubali mapendekezo ya matumizi ya shilingi **154,035,109,000** kwa Wizara ya Afya, (Fungu H01). Kati ya hizo shilingi **35,109,700,000** kwa ajili ya mishahara, shilingi **53,501,100,000** kwa matumizi uendeshaji wa ofisi; na shilingi **4,698,800,000** kwa taasisi zinazopokea ruzuku. Aidha, waidhinishe matumizi ya shilingi **60,725,509,000** kwa kazi za maendeleo, kati ya hizo shilingi **25,194,795,000** kutoka serikalini na shilingi **35,530,714,000** kutoka kwa washirika wa maendeleo.

114. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa hospitali ya Mnazi Mmoja (Fungu H02) naomba wajumbe wa Baraza hili waidhinishe mapendekezo ya shilingi **34,186,349,000;** kati ya hizo shilingi **14,694,200,000** kwa ajili ya mishahara, shilingi **5,969,930,000** kwa matumizi ya shughuli za uendeshaji na shilingi **13,522,219,000** kwa kazi za maendeleo ambapo shilingi **5,553,000,000** kutoka serikalini na shilingi **7,969,219,000** kutoka kwa washirika wa maendeleo. Kwa ufafanuzi zaidi angalia **kimbatisho namba 2**.

115. **Mheshimiwa Spika,** naomba pia Baraza hili liridhie makusanyo ya shilingi **25,000,000,000** kwa Fungu la Wizara (H01) na shilingi **1,000,000,000** kwa Hospitali ya Mnazi Mmoja (H02) kutoka katikavyanzo vya ukusanyaji wa mapato kwa ajili ya kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali.

116. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.



**NASSOR AHMED MAZRUI (MBM)**
**WAZIRI WA AFYA,**
**ZANZIBAR.**

## *Kiambatisho Namba 1:* Muhtasari wa Matumzi kwa Wizara ya Afya (Julai, 2021 - Machi, 2022)

| Programu Kuu/Programu Ndogo | Fungu | Makisio ya mwaka 2021/2022 | Makisio ya Fedha Julai, 2021 - Machi, 2022 | Fedha zilizopatikana (Julai, 2021 - Machi, 2022) | Asilimia ya Fedha Iliyopatikana (Julai, 2021 - Machi, 2022) | Asilimia ya Fedha Iliyopatikana kwa mwaka 2021/2022 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Programu ya Kinga na Elimu ya Afya (PH0301)** | | | | | | |
| PH01: Kinga na Elimu ya Afya | Mishahara | 12,422,400,000 | 9,316,800,000 | 9,775,792,970 | 105 | 78.7 |
| | Matumizi mengine (OC) | 7,732,266,000 | 6,380,753,280 | 833,132,003 | 13 | 10.8 |
| | Fedha za Maendeleo (SMZ) | 2,713,545,000 | 2,492,396,624 | - | - | - |
| | Fedha za Maendeleo (Mhisani) | 11,702,601,000 | 11,273,015,292 | - | - | - |
| | **JUMLA** | **34,570,812,000** | **29,462,965,196** | **10,608,924,973** | **36** | **30.7** |
| **PH02: Programu ya Tiba (PH0302)** | | | | | | |
| PH0201: Programu ndogo ya Huduma za Matibabu | Mishahara | 4,984,800,000 | 3,738,600,000 | 3,681,423,867 | 98 | 73.9 |
| | Matumizi mengine (OC) | 28,710,164,000 | 26,750,813,080 | 10,667,764,446 | 40 | 37.2 |
| | Fedha za Maendeleo (SMZ) | 76,379,946,000 | 55,450,045,000 | 4,724,064,156 | 9 | 6.2 |
| | Fedha za Maendeleo (Mhisani) | 6,900,000,000 | 4,900,000,000 | 4,357,638,389 | 89 | 63.2 |
| | **Jumla ndogo** | **116,974,910,000** | **90,839,458,080** | **23,430,890,858** | **26** | **20.0** |
| PH0202: Programu ndogo ya Huduma za Uchunguzi | Ruzuku (Mshahara) | 1,858,200,000 | 1,393,650,000 | 1,188,716,895 | 85 | 64.0 |
| | Ruzuku (Matumizi ya kawaida) | 1,872,826,000 | 1,220,782,202 | 403,146,213 | 33 | 21.5 |
| | Fedha za Maendeleo (SMZ) | 2,500,000,000 | 2,000,000,000 | - | - | - |
| | Fedha za Maendeleo (Mhisani) | - | 745,030,500 | - | - | - |
| | **Jumla ndogo** | **6,231,026,000** | **5,359,462,702** | **1,591,863,108** | **30** | **25.5** |
| | **JUMLA** | **123,205,936,000** | **96,198,920,782** | **25,022,753,966** | **26** | **20.3** |

## *. . . Kiambatisho Namba 1:* Muhtasari wa Matumzi kwa Wizara ya Afya (Julai, 2021 - Machi, 2022)

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Programu ya Uratibu wa Wizara ya Afya (PH0303)** | | | | | | |
| PH0301: Programu ndogo ya Uongozi na Utawala | Mishahara | 4,062,180,000 | 3,046,635,000 | 2,683,240,350 | 88 | 66.1 |
| | Matumizi mengine (OC) | 4,272,871,000 | 3,986,942,210 | 1,794,352,931 | 45 | 42.0 |
| | Fedha za Maendeleo (SMZ) | - | - | - | - | - |
| | Fedha za Maendeleo (Mhisani) | - | - | - | - | - |
| | **Jumla ndogo** | **8,335,051,000** | **7,033,577,210** | **4,477,593,281** | **64** | **53.7** |
| PH0302: Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti | Mishahara | 910,348,000 | 682,761,000 | 439,905,950 | 64 | 48.3 |
| | Matumizi mengine (OC) | 1,327,816,000 | 1,161,382,877 | 42,000,000 | 4 | 3.2 |
| | Fedha za Maendeleo (SMZ) | 1,500,000,000 | 1,300,000,000 | - | - | - |
| | Fedha za Maendeleo (Mhisani) | - | - | - | - | - |
| | **Jumla ndogo** | **3,738,164,000** | **3,144,143,877** | **481,905,950** | **15** | **12.9** |
| PH0303: Programu ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Afya Pemba | Mishahara | 13,257,232,000 | 9,942,924,000 | 9,794,645,593 | 99 | 73.9 |
| | Matumizi mengine (OC) | 256,000,000 | 84,442,500 | 380,000,000 | 450 | 148.4 |
| | Fedha za Maendeleo (SMZ) | - | - | - | - | - |
| | Fedha za Maendeleo (Mhisani) | - | - | - | - | - |
| | **Jumla ndogo** | **13,513,232,000** | **10,027,366,500** | **10,174,645,593** | **101** | **75.3** |
| | **JUMLA (PH0303)** | **25,586,447,000** | **20,205,087,587** | **15,134,144,824** | **75** | **59.1** |
| | **Miradi ya IMF** | **81,599,563,153** | **45,111,083,897** | **24,413,483,412** | **54** | **29.9** |
| | **JUMLA FUNGU H03** | **183,363,195,000** | **190,978,057,462** | **75,179,307,175** | **39** | **41.0** |

## . . . *Kiambatisho Namba 1:* Muhtasari wa Matumzi kwa Wizara ya Afya (Julai, 2021 - Machi, 2022)

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Hospitali ya Mnazi Mmoja (H02)** | | | | | | |
| PH0201: Programu ndogo ya Huduma za Uchunguzi na Matibabu | Mishahara | - | - | | | |
| | Matumizi mengine (OC) | 813,382,000 | 644,592,750 | 650,724,000 | 101 | 80.0 |
| | Fedha za Maendeleo (SMZ) | - | - | | | |
| | Fedha za Maendeleo (Mhisani) | - | - | | | |
| | **Jumla ndogo** | **813,382,000** | **644,592,750** | **650,724,000** | **101** | **80.0** |
| PH0202: Programu ndogo ya Uongozi na Utawala | Mishahara | 14,808,900,000 | 11,106,675,000 | 10,747,998,600 | 97 | 72.6 |
| | Matumizi mengine (OC) | 4,748,918,000 | 3,589,215,990 | 1,000,000,000 | 28 | 21.1 |
| | Fedha za Maendeleo (SMZ) | - | - | | | |
| | Fedha za Maendeleo (Mhisani) | - | - | | | |
| | **Jumla ndogo** | **19,557,818,000** | **14,695,890,990** | **11,747,998,600** | **80** | **60.1** |
| | **JUMLA KUU HOSPITALI YA MNAZI MMOJA (H02)** | **20,371,200,000** | **15,340,483,740** | **12,398,722,600** | **81** | **60.9** |
| | **JUMLA KUU WIZARA YA AFYA** | **203,734,395,000** | **161,207,457,305** | **87,578,029,774** | **54** | **0.0** |

## *Kiambatisho Namba 2:* Muhtasari wa Makusanyo ya Wizara ya Afya (Julai, 2021- Machi, 2022)

| Kifungu | GFS code | Maelezo | Makusanyo Halisi 2020/2021 | Makadirio ya Makusanyo 2021/2022 | Fedha Zilizokusanywa (Julai, 2021 - Machi, 2022) | Asilimia ya Makusanyo kwa mwaka 2021/2022 | Makadirio ya Makusanyo April Juni, 2022 | Makadirio ya Makusanyo 2022/2023 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| H0301 | **Programu ya Kinga na Elimu ya Afya (PH0301)** | | | | | | | |
| | 142200 | Administration Fees | - | - | - | - | - | - |
| | 1422035 | Shahada ya maradhi | 2,364,420,841 | 2,300,720,000 | 48,059,344 | 2 | 752,000,000 | 118,000,000 |
| | 1422050 | Ada ya uchunguzi wa vyombo vya usafiri na abiria | 26,374,100 | 80,650,000 | 88,071,344 | 109 | 20,348,751 | 64,000,000 |
| | 1422051 | Uchunguzi wa afya ya wafanyakazi | 50,316,200 | 80,603,000 | 58,153,626 | 72 | 18,654,595 | 96,000,000 |
| | | Ukodishwaji wa maeneo ya kibiashara -RCH | - | - | - | - | - | 15,000,000 |
| | | Ukodishwaji wa maeneo ya kibiashara Malaria | - | - | - | - | - | 8,000,000 |
| | 1422078 | Ukodishwaji wa maeneo ya kibiashara UKIMWI | - | - | - | - | - | 10,000,000 |
| | | UVIKO 19 | - | - | 32,447,359,031 | - | - | 24,191,000,000 |
| | **Jumla ndogo** | | **2,441,111,141** | **2,461,973,000** | **32,641,643,345** | | **791,003,346** | **24,502,000,000** |
| H0302 | **Programu ya Tiba (PH0302)** | | | | | | | |
| | 1422095 | Ada ya kibali cha tiba asili | 126,603,142 | 93,952,000 | 27,703,500 | 30 | 25,419,499 | 60,000,000 |
| | 1422118 | Usajili na leseni kwa Wauguzi | - | 116,210,000 | 26,172,440 | 23 | 25,664,669 | 57,000,000 |
| | 1422118 | Usajili na leseni kwa Madaktari | - | 130,000,000 | 59,813,457 | 46 | 26,400,000 | 70,000,000 |
| | 1422118 | Usajili na leseni kwa wataalamu Afya ya Mazingira | - | 182,001,000 | 28,976,457 | 16 | 43,630,954 | 15,000,000 |
| | 1422118 | Usajili na leseni kwa Huduma za Hospitali Binafsi | - | 250,963,000 | 40,550,000 | 16 | 56,000,000 | 100,000,000 |
| | 1422118 | Baraza la wataalamu wa maabara | - | - | | | | 60,000,000 |
| | **Jumla ndogo** | | **126,603,142** | **773,126,000** | **183,215,854** | **24** | **177,115,122** | **362,000,000** |
| H0305 | **Programu ya Uratibu wa Sera za Afya na Utawala** | | | | | | | |
| | 1422084 | Nyaraka za Zabuni | 11,493,379 | 70,000,000 | 86,472,919 | 124 | 17,300,000 | 71,000,000 |
| | 1422094 | Taasisi ya Utafiti wa Afya | - | 105,904,000 | 49,735,506 | 47 | 25,168,750 | 45,000,000 |
| | 1422051 | Huduma za uchunguzi wa afya Pemba | 15,029,780 | 726,950,000 | 9,075,000 | 1 | 181,738,000 | 20,000,000 |
| | **Jumla ndogo** | | **26,523,159** | **902,854,000** | **145,283,425** | **16** | **224,206,750** | **136,000,000** |
| **JUMLA KUU FUNGU H03** | | | **2,594,237,442** | **4,137,953,000** | **32,970,142,624** | | **1,192,325,217** | **25,000,000,000** |

## ... *Kiambatisho Namba 2:* Muhtasari wa Makusanyo ya Wizara ya Afya (Julai, 2021- Machi, 2022)

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Fungu - H02** | | | | | | | | |
| | **Huduma za Uongozi na Utawala (PH0303)** | | | | | | | |
| **H0201** | 1422073 | Malipo ya huduma za afya kwa wagonjwa wa Bima | 48,975,040 | 243,915,000 | 321,339,129 | 132 | 56,662,750 | 591,360,000 |
| | 1422078 | Ukodishaji wa maeneo ya Kibiashara | - | 7,440,000 | 4,557,500 | 61 | 1,860,000 | 8,640,000 |
| | **Huduma za Uchunguzi na matibabu** | | | | | | | |
| **H0202** | 1422094 | Mapato ya utafiti | - | 248,729,000 | 115,543,605 | - | 66,500,000 | 200,000,000 |
| | 1423003 | Kitengo cha huduma za haraka | 749,220,810 | 879,716,000 | 147,997,496 | - | 220,281,588 | 200,000,000 |
| **Jumla H02** | **Jumla ndogo** | | **798,195,850** | **1,379,800,000** | **589,437,730** | **43** | **345,304,338** | **1,000,000,000** |
| **JUMLA KUU WIZARA YA AFYA (H03 & H02)** | | | **3,392,433,292** | **5,517,753,000** | **33,559,580,354** | | **1,537,629,555** | **26,000,000,000** |

## *Kiambatisho Namba 3:* Mchanganuo wa Maombi ya Fedha kwa mwaka 2022/23

| Maelezo | Matumizi ya Maendeleo | | | | Matumizi Mengineyo | | Jumla Kuu |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Mchango wa Serikali | Msaada Washirika wa | Mkopo | Jumla Fedha za Maendeleo | Mshahara | Matumizi ya Kawaida | |
| **Programu ya Kinga na Elimu ya Afya (PH0101)** | | | | | | | |
| Huduma za Kinga na Elimu ya Afya | | | | | 13,095,316,000 | 9,106,854,000 | **22,202,170,000** |
| Mradi Shirikishi wa UKIMWI, Homa ya Ini, Kifua Kikuu na Ukoma | 94,288,000 | 4,944,315,000 | - | **5,038,603,000** | - | - | **5,038,603,000** |
| Mradi wa Kumaliza Malaria Zanzibar | 513,352,000 | 3,422,422,000 | - | **3,935,774,000** | - | - | **3,935,774,000** |
| Mradi Shirikishi wa Huduma za Afya ya Mama na Mtoto | 1,517,588,000 | 1,715,978,000 | - | **3,233,566,000** | - | - | **3,233,566,000** |
| **Jumla** | **2,125,228,000** | **10,082,715,000** | **-** | **12,207,943,000** | **13,095,316,000** | **9,106,854,000** | **34,410,113,000** |
| **Programu ya Tiba (PH0102)** | | | | | | | |
| Programu ndogo ya matibabu (SH0201) | | | | | 5,167,009,000 | 37,726,550,000 | **42,893,559,000** |
| Programu ndogo ya uchunguzi (SH0202) | | | | | 1,728,563,560 | 1,771,136,440 | **3,499,700,000** |
| Mradi wa Ujenzi wa Bohari Kuu Pemba | 3,500,000,000 | - | - | **3,500,000,000** | | | **3,500,000,000** |
| Ujenzi wa Maabara ya Wakala wa Chakula na Dawa | 4,469,567,000 | - | - | **4,469,567,000** | | | **4,469,567,000** |
| Ujenzi wa Hospitali ya Wete | 100,000,000 | 3,648,000,000 | - | **3,748,000,000** | | | **3,748,000,000** |
| Uwekezaji wa Miradi ya Wananchi | - | - | 10,300,000,000 | **10,300,000,000** | | | **10,300,000,000** |
| Ujenzi wa Hospitali ya Mahonda | - | 11,500,000,000 | - | **11,500,000,000** | | | **11,500,000,000** |
| Bima ya Afya Zanzibar | 1,549,893,000 | - | - | **1,549,893,000** | | | **1,549,893,000** |
| Programu ya Kuimarisha Miundombinu ya afya | 8,950,107,000 | - | - | **8,950,107,000** | | | **8,950,107,000** |
| **Jumla** | **18,569,567,000** | **15,148,000,000** | **10,300,000,000** | **44,017,567,000** | **6,895,572,560** | **39,497,686,440** | **90,410,826,000** |

## ... *Kiambatisho Namba 3:* Mchanganuo wa Maombi ya Fedha kwa mwaka 2022/23

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara (PH0103)** | | | | | | | |
| Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji (SH010301) | - | - | - | - | 3,708,640,200 | 5,334,370,800 | **9,043,011,000** |
| Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti (SH010302) | - | - | - | - | 487,207,800 | 1,108,921,200 | **1,596,129,000** |
| Programu ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Afya Pemba (SH010303) | - | - | - | - | 12,651,527,000 | 304,203,000 | **12,955,730,000** |
| Programu ndogo ya Tafiti za Afya (SH010304) | - | - | - | - | 477,300,000 | 642,000,000 | **1,119,300,000** |
| Ujenzi wa Maabara ya Bio-Chemistry | 4,500,000,000 | - | - | **4,500,000,000** | - | | **4,500,000,000** |
| **Jumla** | **4,500,000,000** | **-** | **-** | **4,500,000,000** | **17,324,675,000** | **7,389,495,000** | **29,214,170,000** |
| **JUMLA FUNGU H01** | **25,194,795,000** | **25,230,715,000** | **10,300,000,000** | **60,725,510,000** | **37,315,563,560** | **55,994,035,440** | **154,035,109,000** |
| **Hospitali ya Mnazi Mmoja (Fungu H02)** | | | | | | | |
| Programu ndogo ya Uchunguzi na Matibabu (SH0201) | - | - | - | - | - | 1,140,529,000 | **1,140,529,000** |
| Programu ndogo ya Uongozi na Utawala (SH0202) | - | - | - | - | 14,694,200,000 | 4,829,401,000 | **19,523,601,000** |
| Mradi wa Kupandisha Hadhi hospitali ya Mnazi Mmoja | 5,553,000,000 | 7,969,219,000 | - | **13,522,219,000** | - | - | **13,522,219,000** |
| **JUMLA FUNGU H02** | **5,553,000,000** | **7,969,219,000** | **-** | **13,522,219,000** | **14,694,200,000** | **5,969,930,000** | **34,186,349,000** |
| **JUMLA KUU H01 & H02** | **30,747,795,000** | **33,199,934,000** | **10,300,000,000** | **74,247,729,000** | **52,009,763,560** | **61,963,965,440** | **188,221,458,000** |

*Kiambatisho Namba 4:* **Wagonjwa waliokutwa na Vimelea vya Malaria kwa kipindi cha Octoba, 2021 - Machi, 2022**

| District | Malaria Cases Notified | Malaria cases Investigated | Proportion (%) |
|---|---|---|---|
| Magharibi B | 684 | 586 | 85.7 |
| Mjini | 433 | 404 | 93.3 |
| Magharibi A | 426 | 343 | 80.5 |
| Kati | 384 | 320 | 83.3 |
| Kaskazini A | 202 | 187 | 92.6 |
| Kusini | 155 | 137 | 88.4 |
| Kaskazini B | 151 | 136 | 90.1 |
| Wete | 137 | 134 | 97.8 |
| Chakechake | 79 | 74 | 93.7 |
| Micheweni | 79 | 76 | 96.2 |
| Mkoani | 50 | 45 | 90.0 |
| **Total** | **2,780** | **2,442** | **87.8** |

*Kiambatisho Namba 5:* **Wajawazito, Vizazi, na Vifo vya Mama na Watoto kwa kipindi cha Julai 2020 - Machi 2021 ya Mwaka 2021/2022**

| Wilaya | Wajawazito wa hudhurio la kwanza | Vifo vitokanavy o na Uzazi | Wajawazito waliojifung ua vituo vya Afya | Waliojifung ua kwa upasuaji | Watoto wachanga waliofariki ndani ya siku 7 | Watoto Walizaliwa Mfu |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Chakechake | 4163 | 5 | 4054 | 422 | 12 | 96 |
| Kaskazini A | 4066 | 2 | 3469 | 284 | 27 | 89 |
| Kaskazini B | 2305 | 0 | 362 | 0 | 0 | 3 |
| Kati | 3265 | 1 | 711 | 0 | 0 | 14 |
| Kusini | 1487 | 1 | 1145 | 104 | 2 | 33 |
| Magharibi A | 6130 | 0 | 1202 | 98 | 0 | 9 |
| Magharibi B | 6720 | 2 | 1665 | 186 | 6 | 25 |
| Micheweni | 3375 | 5 | 2922 | 182 | 14 | 56 |
| Mjini | 8843 | 26 | 16360 | 2701 | 301 | 438 |
| Mkoani | 2971 | 4 | 2424 | 246 | 66 | 71 |
| Wete | 3870 | 4 | 2898 | 288 | 41 | 60 |
| **Total** | **47195** | **50** | **37212** | **4511** | **469** | **894** |